

# *WAEBRANIA, MLANGO WA SITA* <sup>2</sup>

 . . . kusoma Neno Lake la thamani.

Niliingia, muda mfupi uliopita, nami nilikuwa nimebeba Biblia mbili. Nami nilikuwa na mazungumzo mafupi na bibi mmoja hapa aliyeko kule nyuma, basi nikamwambia kama ningehubiri kutoka kwenye zote mbili, tunapaswa kuwa na somo zuri sana. Lakini hii ni kamusi ya Kiyunani, kwa hiyo ni kitu fulani tu ninachotaka kusoma kutoka kwenye hii, usiku wa leo. Nininii—ni ninii . . . Ni tafsiri ya neno kwa neno, kutoka kwenye Kiyunani cha awali, kwenda Kiingereza. Nayu imekuwa ni msaada mkubwa sana kwangu toka kipengee hadi kipengee. Nami ninataka tu kusoma kitu fulani toka katika hilo, kwa maana sasa tunabukua katika Kitabu hiki cha Waebrania, na tunafikia kwenye maana halisi za kina.

<sup>219</sup> Nami nilimwambia Ndugu Neville, dakika chache zilizopita, “Tunaingia kwenye sehemu ambayo watu wanakuna vichwa vyao na kusema, “Siamini jambo hilo.” Unaona? Hiyo ndiyo aina tunayoingilia. Hapo ndipo tunapopenda jambo hilo.

<sup>220</sup> Mhudumu fulani aliniambia, alisema, “Vema, nadhani kutakuwapo na kujikuna kichwa kwingi sana.”

<sup>221</sup> Nikasema, “Hivyo ndivyo tunavyotaka kufanya.” Unaona?

<sup>222</sup> Biblia inaweza kuwa na maana moja tu. Haiwezi kuwa na maana mbili. Na kama sehemu moja ya Biblia inasema jambo moja, na sehemu nyingine ya Biblia inasema jambo lingine, basi kuna kitu kasoro. Unaona? Haina budi kusema jambo hilo, kila mahali. Lakini, kumbuka, katika kuisoma Biblia, “Imefichwa kwa macho ya wenyewe hekima na akili, na imefunuliwa kwa watoto wachanga,” kwa kuwa ni Kitabu cha kiroho.

<sup>223</sup> Wala si kitabu cha magharibi. Ni Kitabu cha mashariki. Na kuna kitu kimoja tu kinachoweza kukifasiri, na huyo ni Roho Mtakatifu. Ninajua ya kwamba kila mmoja wetu anataka kusema, ya kwamba, “Roho Mtakatifu anatwambia kile tunachoamini ndani ya Hilo.” Vema, sasa, kama kila Andiko linaafikiana barabara namna ile ile, basi huyo ni Roho Mtakatifu. Kama haliafikiani, na lina mwanya *hapa*, na mwanya *huku*, basi kuna kasoro fulani na imani yetu. Na, loo, ni Kitabu cha ajabu sana.

<sup>224</sup> Sasa, ninawatakeni mfanye hivi wakati tukijifunza. Sasa, inatubidi kuondoka asubuhi na mapema kwenda Wyoming, Bwana akipenda. Tuombeeni.

Na juma hili lijalo, Ndugu Graham Snelling, hapa . . . Yupo. Nilimsikia, dakika chache tu zilizopita, akitangaza tangazo lake. Na kanisa hili linashirikiana kikamilifu na ufufuo wake.

Nasi tunamwomba Mungu, apate kumpa ufuluo mkuu mno na mzuri. Ndugu Graham aliendesha ufuluo kwa ajili ya Ndugu... hapa Charlestown, Ndugu Junior Cash, na kulipatikana papo hapo waongofu mia moja, ninaamini. [Mtu fulani anasema, "Themanini na nne."—Mh.] Waongofu themanini na nne. Kwa hiyo, kwa jambo hilo, tunamtukuza Mungu. Nasi tunatumaini ya kwamba kutakuwako na mia tano na themanini na nne hapa, mahali hapa.

<sup>225</sup> Ndugu Graham alikutana nami leo, na akasema, "Sasa, Ndugu Bill, nina hakika ya kwamba unaelewa kwamba mimi siko hapa kuanzisha kazi nyininge kupinga maskani, kwa kuwa mimi ni sehemu ya maskani." Yeye yupo hapa tu kuninii... Anajisikia moyoni mwake ya kwamba anataka kuendesha uamsho, na Bwana anamwongoza kufanya hivyo. Na—naye anawaalika waongofu, na ana kanisa, la kuwamiminia mle, "Hilo hapo kanisa la nyumbani, kama ukiingia humo, ongoka."

<sup>226</sup> Na ni jukumu letu, kama Wakristo, kumuunga mkono na kila kitu tuwezacho kumuunga mkono nacho. Na Bwana na ambariki Ndugu Graham. Na ninyi, kila mmoja wenu, mnaalikwa kwa furaha kwenye mkutano wa Ndugu Graham hapa, kwa ruhusa kamili kutoka kwenye kanisa hili, kwa ushirikiano mkamilifu kumsaidia kwa njia yoyote tuwezayo, kwa ajili ya nafsi zilizopotea na kwa ajili ya Ufalme wa Mungu.

<sup>227</sup> Bwana akubariki, Ndugu Graham, akupe mikutano mizuri sana. Yeye hajui ni lini atakapofunga. Ndio tu anaanza. Na kwa hiyo, Ndugu Graham amepata shida kama mimi, *mema* na *mabaya* mengi. Hivyo ndivyo maisha yanavyoenda. Inakufanya kuthamini yale *mema* baada ya kupitia kwenye hayo *mabaya*. Kama mtu akianguka na kukaa pale, yeye ni mwoga. Nina imani wakati mtu atainuka na kujaribu tena. Hiyo ni kweli. Nina hakika mnaweza kufafanua ninayomaanisha. Sasa, msisahau hilo, juma hili lijalo.

<sup>228</sup> Sasa, katika Kitabu hiki cha Waebrania, hatutachukua msingi usiku wa leo.

<sup>229</sup> Sasa, Jumapili ijayo, Bwana akipenda, Ndugu Neville atatangaza. Ndugu Cox hapa, ama baadhi yao, watamjulisha, iwapo tuwahi kuingia kwa ajili ya mkutano wa Jumapili ijayo. Atatangaza jambo hilo kwenye redio. Nasi tunaninii... Ninyi nyote isikilizeni redio yake sasa, na—na—na waalikeni majirani wenu wote kusikiliza. Kwa kweli mimi hupata furaha katika kusikiliza mahubiri yao na kuimba, ile kwaya ya watu wanne ya akina Neville. Sisemi jambo hilo kwa sababu yeye ameketi hapa. Kama ningalisema jambo hilo, na sikumaanisha hivyo moyoni mwangu, ningekuwa ni mnafiki. Hiyo ni kweli. Ingenibidi kutubu. Lakini ninamaanisha. Nami ni afadhali nimpe tumba dogo la waridi sasa kuliko shada zima akiisha kuaga dunia.

<sup>230</sup> Wakati mmoja nilikuwa nikitoka pale mlangoni, na kulikuwako na bibi mmoja aliyenijia, naye akasema, “Ndugu Branham, loo, jinsi nilivyofurahia ule ujumbe!”

<sup>231</sup> Nikasema, “Asante.” Ikanifanya kujisikia vizuri.

<sup>232</sup> Mtu mwingine akaja, akasema, “Ndugu Branham, ninafurahia Ujumbe ule.”

<sup>233</sup> Nikasema, “Asante.”

<sup>234</sup> Kulikuwako pale na maskini mhubiri mmoja, kutoka sehemu hizi huku za kaskazini mwa nchi, mkoani, akasema, “Mungu atukuzwe, mimi sitaki watu wanijivunie namna hiyo.”

<sup>235</sup> Nikasema, “Mimi ninapenda wanijivunie.” Halafu nikasema, “Kuna tofauti moja tu kati yangu mimi na wewe. Mimi ni mnyofu juu ya jambo hilo.” Hiyo ni kweli. Sisi sote tunapenda kusikia maneno mazuri yakisemwa juu yetu. Na mimi—nafikiri ni vizuri sana kusema mambo mazuri juu ya huo. Na kama unataka mtu fulani aseme maneno mazuri juu yako, sema maneno mazuri juu ya mtu mwingine. Hivyo ndivyo unavyopaswa kufanya jambo hilo, ndipo daima utasema mambo mazuri sana uwezayo juu ya kila mtu. Na hilo linalifanya gurudumu kuvungirika vizuri zaidi.

<sup>236</sup> Sasa, kuhusu jambo hili, Jumapili ijayo, Bwana akipenda, kwa maoni yangu, tunaninii, tunaendelea kuzama zaidi na zaidi katika siri hizi kuu za Mungu. Tunaingia kwa Melkizedeki: Yeye alikuwa ni nani, alitoka wapi, alienda wapi, nini kilitukia Kwake, na yote kuhusu Melkizedeki.

<sup>237</sup> Na sasa, usiku wa Jumatano iliyopita, Ndugu Neville aligusia mlango wa kumalizia wa ukuu wa Uungu na ukuhanini wa Bwana wetu Yesu, ambao unaanzia hapo mwanzo, “Mungu, katika nyakati nyingi na kwa njia nyingi alinena na baba zetu katika manabii, katika siku hii ya mwisho amesema nasi katika Mwanawе, Kristо Yesu.”

<sup>238</sup> Halafu anaendelea, na anaanza kuelezea na kuleta picha kwamba Yeye alikuwa ni nani, anamleta hadi kwenye mlango wa 5, mwishoni mwa mlango wa 5.

<sup>239</sup> Halafu kuanzia kwenye mlango wa 6, tulipata jambo hili kwenye somo letu la asubuhi ya leo.

*Kwa sababu hiyo, tukiacha kuyanena mafundisho ya kwanza ya Kristо, tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu; . . .*

<sup>240</sup> Ni wangapi waliofurahia ule ujumbe juu ya utimilifu? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] “Na tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu.” Huo ulikuwa ndio Ujumbe wetu, asubuhi ya leo, katika sura ya 6 ya Waebrania.

<sup>241</sup> Basi tunafikia sasa mahali ambapo tunaanza kupata se—sehemu yenye hasa. Loo, sote tunaweza kukubaliana juu

ya mambo haya: juu ya Uungu wa Kristo; na Yeye akiwa ni Mwana wa Mungu; na jinsi Yeye alivyokuwa pamoja na Mungu, na Mungu alivyokuwa pamoja Naye; Naye alikuwa ndani ya Mungu, na Mungu alikuwa ndani Yake, na kadhalika. Sote tunakubaliana juu ya hayo. Lakini, sasa, kutoka hapa na kuendelea, sijui jinsi gani tutakavyokubaliana. Kwa hiyo chochote kile kiwacho, kila siku chache usiku, tutawapa nafasi na mniandikie maoni mafupi na mniambie mnavyowazia juu Yake.

<sup>242</sup> Ndipo itanibidi kujibu maswali. Na kama siwezi kuyajibu, nitasema, “Ndugu Neville, unasemaje juu ya jambo hilo?” Nitasema, “Huyo hapo. Acheni alijibu.” [Ndugu Neville anasema, “Hapo ndipo nitakaposoma lile la Kiyunani.”—Mh.] Hapo ndipo atakaposoma kamusi, atoe la Kiyunani. Nafikiri wakati umewadnia wa mimi kufanya hivyo, pia.

<sup>243</sup> Lakini, sasa, kama tukiazimia na kuwa waaminifu kabisa, na kweli tuje kwa ajili ya kusudi moja, nalo ni, kujifunza. Mimi pia ninataka kujifunza. Nayo Biblia imeandikwa, ilisema, “Ni... Maandiko si ya kufasiriwa apendavyo mtu fulani.” Hiyo inamaanisha Andiko halina budi kufasiri Andiko. Unaona? Kila Andiko linapaswa kufasiri hilo lingine, katika Biblia nzima, kuifanya kuwa kitu kimoja kikuu. Kwa sababu, Mungu hawezi kubadilika, kwa kuwa Yeye ni Mungu asiyebadilika.

<sup>244</sup> Sasa, “Tukiacha...”

*Kwa sababu hiyo, tukiacha kuyanena mafundisho ya kwanza ya Kristo, tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu;...*

<sup>245</sup> Ninampenda Paulo akisema mambo hayo. Paulo kamwe hakuwa mtu aliyependa kukaa muda mrefu sana mahali pamoja. Alipenda kusonga mbele, kwenye kina zaidi. Wakati mmoja, katika Maandiko, alisema, “Mimi, nikiyasahau mambo hayo yaliyo nyuma, ninapiga mbio kuifikilia mede ya wito mkuu.” Unaona? Yeye anaendelea kusonga mbele.

<sup>246</sup> Hapa ye ye alisema:

*Sasa tukisahau kuyanena mafundisho ya kwanza ya Kristo (kwamba alikuwa ni nani, alikuwa nini), hebu tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu;...*

<sup>247</sup> Sasa sisi, kwanza, tulitaka kujua, “Je! tungeweza kuwa *wakamilifu?*” Nasi tuliona ya kwamba, katika Maandiko asubuhi ya leo, Mathayo 5:28, ya kwamba Yesu alisema ya kwamba sisi “ilibidi tuwe wakamilifu tu kama vile Mungu alivyuo mkamilifu,” la sivyo hatutaingia.

<sup>248</sup> Ndipo tukakuta kwamba tulikuwa, kila mmoja, “tulizaliwa katika dhambi, tukaumbwa katika uovu, tukaja ulimwenguni tukisema uongo.” Na hakuwa na kitu kimoja chema sisi tulichokuwa, kwa hiyo tungeweza kupata kukamilishwa?

<sup>249</sup> Sasa hapa ndipo tunapoona basi, huku, tukisoma, tukichukua Andiko kwa Andiko, ya kwamba, “Yesu, kwa dhabihu moja, alikamilisha, milele, Kanisa Lake.” Yeye... Sisi basi ni wakamilifu, kwa njia ya Kristo. Nasi tuko huru na hukumu, kwa njia ya Kristo. Hatutakufa kamwe, katika Kristo. Tumepoteza mauti na tukapata Uzima, katika Kristo; si kwa kanisa lolote, si kwa madhehebu yoyote, si kwa mazingaombwe yoyote, si kwa kunena kwa lugha, si kwa kupiga makelele, si kwa kutetemeka, si kwa kuchenza katika Roho, bali ni kwa neema.

<sup>250</sup> Mungu huita Yeye atakaye. Na yote ni kwa kuteuliwa, tunaona. Tunaona, ya kwamba, “Si kwa uwezo wake yeye anayetaka kuokolewa. Si yeye atakaye wala yeye apigaye mbio; ni Mungu arehemuye.” “Wala hakuna mtu anayeweza kumjia Yesu asipovutwa na Mungu, kwanza.” Kwa hiyo una uhusiano gani na jambo hilo, hata hivyo? Huna uhusiano wowote na jambo hilo. Huko kwenye picha, kabisa.

<sup>251</sup> Tuliona ya kwamba mwanadamu kamwe hamtafuti Mungu. Mungu ndiye anayemtafuta mwanadamu. Pia tuliona, basi, ya kwamba Mungu ndiye chanzo pekee cha Uzima wa Milele. Tuliona ya kwamba kila kitu ambacho ni cha Milele hakina mwanzo wala mwisho. Kwa hiyo, tunaona ya kwamba kuzimu ilikuwa na mwanzo, na ina mwisho. Na kuna ninii tu... Hakuna mtu anayeweza kusema kamwe ya kwamba... Kuzimu ni ya daima, daima, naam, ya daima, bali si ya Milele.

<sup>252</sup> *Daima* ni “kipindi cha wakati.” Biblia inasema, “Kudumu daima.” Na ninyi lichunguzeni na mwone kama *daima* halimaanishi “kipindi cha wakati.” Yona alisema alikuwa katika tumbo la nyangumi “daima.” Na Maandiko mengine mengi, daima inamaanisha tu “kipindi cha wakati.”

<sup>253</sup> Lakini, Milele, hiyo ni pasipo na kikomo, yaani ni kudumu daima na daima na daima na daima. Ni kile kisicho na Mwisho. Nasi tunaona ya kwamba kuzimu si ya Milele, bali ni ya kipindi fulani. Na sababu, inakupassa kuangalia maneno hayo, sasa. Kama hutayaangalia, utachanganyikiwa. Sasa, kumbukeni, ni mambo yale tu yasiyokuwa na mwanzo, ndiyo hayana mwisho. Kwa hiyo, Yesu alisema, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima,” daima? Je! hilo linasikika kuwa sawa? La. “Yuna Uzima wa Milele.” Na neno *Milele* ni “Mungu.” Neno hilo, hili hapa papa hapa katika kamusi ya Kiyunani, Zoe Uzima wa Mungu ndani yako. Nawe ni wa Milele tu kama vile Mungu alivyo wa Milele, kwa maana una Mungu ndani yako.

<sup>254</sup> Tabia yako ya kale ilikufa, ile tabia ya ulimwengu, nawe umekuwa kiumbe kipywa. Na shauku zako, yale maisha ya kale yaliyokuwa na mwanzo wakati Mungu alipopumulia pumzi ndani ya mianzi ya pua yako, ulipozaliwa, ule uhai wa tabia

ya kimwili ulikuwa. Nao ulikuwa na mwanzo na ulikuwa na mwisho, nao ulikuwa na uliangamizwa milele, ile tabia ya kale. Ndipo Mungu akaja na kuingia ndani na ile Tabia mpya. Ndipo, upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, amani, saburi, na upole, na wema, tabia ambayo iliingia; na kuchukua mahali pa kijicho, na hasira, na chuki, na—na wivu, ugomvi, na mambo hayo yote. Illichukua mahali pake, ulipopita toka mautini kuingia Uzimani. Mnalipata, kwa usahihi sana, sasa? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

<sup>255</sup> Kwa hiyo, sikilizeni. Kuna aina moja tu ya Uzima wa Milele. Utambue Huo. Hiyo ni kusema, Mungu pekee ndiye aliye na Uzima wa Milele. Biblia ilisema hivyo. Mungu peke yake ana Uzima wa Milele. Na kama mtu atateseka katika jehanamu, milele, hana budi kuwa na Mungu, Milele. Lakini ninasema jambo hilo hapo.

<sup>256</sup> Sasa, kumbukeni, sisemi ya kwamba hakuna jehanamu inayowaka moto. Kuna jehanamu inayowaka moto, moto na kiberiti. “Ambako bu—buu lake ni...moto hauzimiki na buu halifi kamwe,” ya moto na kiberiti, adhabu. Huenda ikadumu kwa miaka bilioni mia moja. Bali haina budi kuwa na mwisho, kwa maana jehanamu iliumbwa kwa ajili ya Ibilisi na malaika zake. Na kila kitu ambacho Mungu Mwenyewe, wa kweli, aliyekuwako hapo mwanzo, kila kitu kilitokana na Mungu. Wakati roho ile hasa...

<sup>257</sup> Hebu chukua tu *Roho* ya upendo, ambayo ilikuwa ni chemchemi kuu ya Mungu, safi, isiyoghoshiwa. Kutokana na huo, ukaja upendo *uliopotoshwa*. Ndipo unakuja kwenye upendo wa *kibinadamu*. Halafu inakuja kwenye upendo wa *kujuana kimwili*. Halafu unakuja kwenye pendo zingine, pendo na pendo, na unaendelea tu kupotoshwa mpaka unakuwa ni *uchafu* tu. Lakini mambo hayo yote yalikuwa na mwanzo. Na siku moja yataishia moja kwa moja kwenye ile asili yake; ni wa Milele; ambapo ashiki, upendo wa kibinadamu, upendo wa kimapenzi, pendo hizo zote itabidi zikome.

<sup>258</sup> Imani hizi zote za kujifanya itabidi zikome. Kuna Imani moja ya kweli. Nyingine zote itabidi zikome. Zilikuwa ni potovu zilizotokana na chemchemi hii halisi.

<sup>259</sup> Kwa hiyo, basi, kuzimu, mateso, mateso si ya Milele. Mateso yaliletwa kwa sababu ya dhambi, nayo dhambi ikaleta mateso. Na wakati dhambi itakapokwisha, itabidi mateso ya ishe, pia. Na kutakuwako na wakati ambapo wenye dhambi, ambao hawakumkubali Kristo kamwe, baada ya wao kuadhibiwa labda kwa miaka bilioni mia moja,... Sijui, labda kwa miaka milioni mia kumi bilioni, nisingeweza kusema. Bali itabidi yakome, wakati fulani, maana si ya Milele.

<sup>260</sup> Sasa, tutakaza mwendo sasa, tuufikilie utimilifu. Sasa sikilizeni, tunapoingia kwenye Ujumbe.

*...tusiweke msingi tena wa kuzitubia kazi zisizo na  
uhai, na wa na imani kwa Mungu,*

*Na wa mafundisho ya mabatizo, ...kuwekea  
mikono, ...kufufuliwa wafu, na hukumu ya milele.*

<sup>261</sup> Sasa sikilizeni. Tuna mbili. Tuna picha hapa, sasa. Sasa papa hapa ndipo tutakopata ubishi mkali sana. Sasa inakupasa kuona mahali picha hii ilipo. Paulo anajaribu, hapa, kutenganisha torati na neema. Tuna picha mbili: moja, ile ya tamaa za kimwili; moja, ile ya kiroho. Na Paulo anajaribu kutenganisha zote mbili, kuwaonyesha Wayahudi. Waraka huu ni kwa Waebrania. Na Waebrania wote unajaribu kuwaonyesha mfano wa Agano la Kale likiwa mfano wa lile Jipy. Kwa hiyo, una picha mbili hapa zinazonenwa habari zake.

<sup>262</sup> Sasa sikiliza kwa makini tunaposoma. Sasa yeye alisema:

*...tukiacha kuyanena mafundisho ya kwanza ya  
Kristo, tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu; ...*

<sup>263</sup> Sasa, tulipata hilo asubuhi ya leo, jinsi ambavyo tunakamilishwa. Tunakamilishwa, tukawa kabisa bila waa wala lawama, hatuna hata dhambi moja juu yetu. Je! wewe huwezi kujaribiwa? La, hasha. Je! unatenda dhambi kila siku? Naam, bwana. Lakini, hata hivyo, tumekamilishwa kwa sababu tumo ndani Yake. Wala Mungu asingeweza kutuhukumu tena hata kidogo (asingekuwa mwenye haki), Yeye tayari ametuhukumu katika Yeye. Wakati alipomhukumu Kristo: Yeye alinihukumu mimi, alikuhukumu wewe. Wala hawesi kunihukumu tena, kwa maana Yeye alichukua hukumu yangu kama nimekombolewa.

<sup>264</sup> Nami nina risiti ya kuwaonyesha ya kwamba nimeikombo saa yangu kutoka kwenye duka la rehani, hebu mtu fulani ajaribu kuirudisha tena kwenye duka la rehani, wakati nikiwa na risiti. Nimeikombo.

Na kama Ibilisi angejaribu kuweka adhabu juu yangu, nina risiti inayoonyesha ya kwamba nimekombolewa. Naam, bwana. Hakuna hukumu tena! “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele, wala hataingia hukumuni, bali amepita toka mautini kuingia Uzimani.” Hiyo ndiyo risiti yangu. Yeye alitoa hiyo ahadi.

<sup>265</sup> Sasa, sasa hiyo picha, hapa.

*...tusiweke misingi tena wa kuzitubia kazi zisizo na  
uhai, na ...kuwa na imani kwa Mungu,*

*...mafundisho ya ubatizo, ...kuwekea mikono, ...  
kufufuliwa wafu, ...hukumu ya milele.*

<sup>266</sup> Sasa, kumbuka, unaona neno hilo likitumiwa tena? Tulilitumia asubuhi ya leo, “Hukumu ya Milele.” Mungu anenapo mara moja, ni la Milele. Haliwezi kubadilishwa, hata kidogo. Kwa hiyo, hukumu ni ya Milele, daima ni hukumu. Na haidhuru tunaishi katika kizazi kipi, kizazi kimoja kitaishi, na

kimoja... wote wataishi, na ni daima, kwa wakati wowote ule, na *hili* na *lile*. Lakini hukumu ya Mungu ingali ni ya Milele, hana budi kuwa hivyo, kwa maana Yeye alinena hilo Neno. Mungu anaponena Neno, halina budi kuwa ni la Milele. Hiyo ni kweli.

<sup>267</sup> Sasa hebu nisome hilo kutoka kwenye ya Kiyunani kwa ajili yenu. Sikilizeni vile inavyosema.

*Kwa sababu hiyo tukiacha—tukiacha kuyanena mafundisho ya kwanza ya Kristo, yule aliyepatanisha, na tujitahidi—tujitahidi kuelekea kwenye...*

Sasa, siwezi kuyasoma. Yana kiwi. “Na si kuweka tena mfano...” Tumelifikia.

*...sio kuweka tena mfano wa matengenezo kutokana na kazi zinazosababisha mauti.*

<sup>268</sup> Sasa, kamusi hii si ufasiri wowote kamwe, hata kidogo. Ni neno tu la Kiyunani kwa yale Kingereza kinayosema. Na ilisema, “Sasa hatutaki...” Sikilizeni hapa, unaona.

*...sio kuweka tena misingi ya matengenezo kutokana na kazi zinazosababisha mauti.*

<sup>269</sup> Sasa kama utalitunza hilo niani mwako, ambalo anazungumzia hapa, ya kwamba, “Mifano ya matengenezo inasababisha mauti.” Paulo alisema, “Tukiacha kuyanena mafundisho ya kwanza, tuufikilie utimilifu, tusiweke msingi tena wa kuzitubia kazi zisizo na uhai, na kuwa na imani kwa Mungu: mafundisho ya ubatizo, kuwekea mkono, kufufuliwa kwa wafu, hukumu ya Milele. Mfano wa matengenezo yanayosababisha mauti,” yalikuwa ndiyo maneno sahihi. Hivyo ndivyo Paulo alivyoandika hasa. Unaona kile anachojaribu kufanya?

<sup>270</sup> Sasa, mambo haya yote, kama mabatizo: mmoja anabatizwa kichalichali, mmoja kifudifudi, mmoja katika jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, mmoja katika jina la Yesu, mmoja *hivi*, na *vile*, na mambo haya yote mbalimbali madogomadogo ya mabatizo.

<sup>271</sup> Na ya kuwekea mikono: “Mungu asifiwe, nina karama ya kuwekea mikono. Haleluya! Wewe, unaweza kumpata namna *hii*. Haleluya!”

<sup>272</sup> Tukiweka hayo yote kando, kwa maana hizo ni kazi zisizo na uhai, matengenezo haya, kutengeneza. Unaona? Yeye anazungumza juu ya tabaka nytingine. Sasa yeye alisema, “Hebu na tuondokane na hayo, na tukaze mwendo tuufikilie utimilifu.” Unalipata? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

<sup>273</sup> Na kanisa lingali linajikokota huko nyuma kwenye mambo hayo. Hivyo ndivyo walivyokuwa wakijaribu kufanya. Kanisa la Kiebrania la mwanzoni lilikuwa likijaribu kusema, “Vema,

nilibatizwa kwa kuzamishwa, na—na nilipata *hiki*, na *hiki*, na mambo *haya yote*.”

<sup>274</sup> Yeye akasema, “Sasa, wekeni hayo yote kando, mkayaache nyuma.” Lakini, sasa, je! yeye alisema hatupaswi kuyafanya? Sasa sikilizeni yale aliyosema kuhusu mambo hayo.

*Na hayo tutafanya Mungu akitujalia.*

<sup>275</sup> Na lile la awali lilisema jambo lile lile.

*Hayo tutafanya, kama Mungu atatujalia, unaona.*

*Hayo tutafanya, Mungu akitujalia.*

<sup>276</sup> Mabatizo, kuwekea mikono, na kadhalika, bali hayo si makamilifu. Hayo ni matengenezo tu ya kimwili. Na hapo ndipo makanisa yanapocepukia, siku hizi, ni kwenye matengenezo hayo ya kimwili. Moja ya hayo lilisema, “Loo, vema, maji, neno ubatizo linamaanisha *hivi* na linamaanisha *vile*.”

<sup>277</sup> Ndipo wakaanzisha madhehebu: na moja linanyunyizia, hilo lingine linamimina, hilo lingine linabatiza kifudifudi, hilo lingine kichalichali, na mambo hayo yote; mengine yao kuwekea mikono wagonjwa, na mengine kuwafanya mitume, na mengine kuwafanya manabii na kadhalika, kwa kuwekea mikono; na kuhubiri kufufuka toka kwa wafu, na ambayo ni sawa; na Uungu mkuu wa Kristo, hilo ni sawa. “Lakini,” yeye alisema, “yote haya ni matengenezo ya kidesturi. Tumekuwa tu tukitengeneza. Sasa na tukaze mwendo tuufikilie utimilifu.” Mnapata hiyo picha? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

<sup>278</sup> Sasa angalia. Hapa panapokuja sasa ndipo mahali penye jambo la kilindi.

*Kwa maana hao waliokwisha kupewa nuru, na kukionja kipawa cha mbinguni, na kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu,*

*Na kulionja neno zuri la Mungu, . . . nguvu za zamani zijazo,*

*Wakaanguka baada ya hayo, haiwezekani kuwafanya upya tena hata wakatubu; kwa kuwa wamsilibisha Mwana wa Mungu mara ya pili kwa nafsi zao, na kumfedhehi kwa dhahiri.*

<sup>279</sup> Sasa, ninajua yale ninyi washika sheria mnayowazia niani mwenu sasa hivi, lakini mmekosea. Unaona? Vema. Ninasimama kwenye jambo hili, na Biblia inalithibitisha, ya kwamba, “Kama Mungu aliwahi kumwokoa mtu, yeye ameokolewa kwa wakati na Umilele.” Huwezi kulifanya lisema kitu chochote kingine.

<sup>280</sup> Mshika kanuni fulani alinijia, si muda mrefu uliopita, na kusema, “Nimekupata kwenye moja, Mhubiri Branham. Nimekupata kwa moja. Wewe ulisema, ‘Kama mtu alikuwa ameokoka, asingweza kupotea kamwe?’”

<sup>281</sup> Nikasema, “Hivyo ndivyo Mungu alivyosema.”

<sup>282</sup> Akasema, “Ninataka kukuuliza jambo fulani. Sauli alikuwa ni nabii, naye alitabiri. Nawe unajua alikuwa ni mtiwa mafuta wa Mungu. Biblia ilisema alikuwa hivyo. Naye alijiua, na akapotea.”

<sup>283</sup> Nikasema, “Ati alipotea?” Nikasema, “Biblia inathibitisha ‘aliokoka.’ Akiisha kuwa adui wa Mungu, alikuwa akali ameokoka. Biblia ilisema aliokoka. Na, hata hivyo, hakujiuwa. Mfilisti alimwua, ndipo Daudi akamwua huyo Mfilisti kwa kumwua Sauli. Kweli aliangukia upanga wake, mkuki wake, upanga, bali, yeze alifanya hivyo. Huo haukumwua. Ndipo Mfilisti akamwua. Na basi wakati Sauli aliposhuka akaenda kwa yule mchawi, na huyo mwanamke akaiita roho ya Samweli, kwa maana hakuwa ameingia Utukufuni, alikuwa paradiso chini ya damu iliyomwagika ya mafahali na mbuzi ambayo isingweza kuondoa dhambi. Lakini ilibidi awe na mahali pa kungojea, ambapo panaitwa paradiso, mpaka alipoingia.”

<sup>284</sup> Hapo ndipo ninyi Wakatoliki mlipochanganyikiwa. Unaona? Sasa, hakuna paradiso tena sasa. Tunaenda moja kwa moja Uweponi mwa Mungu.

<sup>285</sup> Na wakati yule mchawi wa Endori alipoiita roho ya Samweli, huyo hapo akasimama. Ndipo huyo mwanamke mchawi akaanguka kifudifudi, na kusema, “Kwa nini ulinidanganya?”

<sup>286</sup> Na si kwamba tu Sauli alikuwa amesimama tu pale... Ninamaanisha Samweli, katika mavazi yake ya nabii, yeze alikuwa angali ni nabii. Alisema, “Kwa nini uliniita kutoka kwenye mapumziko yangu,” kasema, “kwa kuwa umekuwa adui wa Mungu?”

<sup>287</sup> Akasema, “Vema, Urimu hazinizingumzii tena. Nabii hawezি kunitabiria tena. Wala siwezi kuota ndoto.”

<sup>288</sup> “Vema,” Samweli akasema, “umekuwa adui wa Mungu. Lakini kesho vita vitaenda vinginevyo, nawe utakuwa kesho. Na kwenye wakati huu, kesho usiku, utakuwa pamoja nami.” Kama Sauli alikuwa amepotea, vivyo hivyo na Samweli pia, wote wawili walikuwa wako pamoja. Hakika. Biblia ilisema hivyo.

<sup>289</sup> Sasa, unaweza kusimikwa sana katika mhemuko, kwa kunena kwa lugha, kupaaza sauti, kushtuka-shtuka, kutetemeka, kukimbia huku na huko kwenye marefu ya kanisa. Sina kitu dhidi ya hayo. Lakini unaweza kujifanya uamini ya kwamba umeokoka wakati hujaokoka, hujaokoka. Maisha yako yatathibitisha kile ulicho. Yesu alisema yatathibitisha, “Kwa matunda yao mtawatambua.” Maisha yako yatathibitisha kama umeokolewa ama hujaokolewa, hata kama hujapata kufungua mdomo wako. Yatathibitisha kile ulicho.

<sup>290</sup> Lakini huku kujichochea kote na kuhemukwa na kujiunga na kanisa, “Na nimebatizwa katika Jina la Yesu, haleluya, ninajua nimempata,” hayo hayamaanishi kitu.

<sup>291</sup> “Nimebatizwa, jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, kifudifudi, mara tatu. Nimempata.” Hayo hayamaanishi kitu.

<sup>292</sup> Paulo alisema, “Na tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu sasa.” Tunanena habari za kukamilishwa. Na kama tutachunguza jambo hili lote, utaona ya kwamba, waliokamilishwa ni wale Wateule. Nitawathibitishia, katika dakika chache, kwa Biblia. Hao wateule ndio ambaao Mungu, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, aliwaona kila mmoja wao. Naye alimtuma Yesu kuwakomboa watu hao, si ulimwengu wote. Alitaka kufanya hivyo, bali ilimbidi kufanya njia kwa ajili ya hao. Na njia pekee angaliweza kutenda hilo, ilikuwa ni kumtuma Kristo; apate kuja, msamaha wa dhambi zetu, kusudi wale ambaao wameteuliwa, angeweza kuwaleta Kwake, Utukufuni.

<sup>293</sup> Ungeweza kuwazia Mungu akiendesha ofisi Yake kizembe hivyo, hivi aseme, “Vema, pengine mtu fulani atanisikitikia sana, labda watakuja na wapate kuokolewa”? Mungu hana haja ya kukusihi kufanya lolote. Kusihi kokote, wewe ndiwe uliye una haja ya kusihi, si Mungu.

<sup>294</sup> Na tena, Kristo alikuwa apate kuwaokoa wale ambaao Mungu, kwa kujua tangu zamani, aliwachagua kukutana Naye huko ng’ambo bila waa wala kunyanzi. Kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, Yeye alikuona Utukufuni. Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema, Waefeso, mlango wa kwanza. Mlango wa 5, kifungu cha 1. Mungu alichagua tangu zamani kwa kujua tangu zamani.

<sup>295</sup> Sasa, kama Mungu alifanya jambo hilo, alituchagua tangu zamani kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu; naye akamjua kila mmoja wetu kwa jina, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu; Naye alituteua tupate Uzima wa Milele; kisha akamtuma Yesu Kristo kutukomboa, yaani, miaka elfu sita iliyopita, Yeye alituona, tupate kutokea kwa ajili ya sifa Zake Utukufuni! Unawezaje kamwe kupotea?

<sup>296</sup> Sasa, kama umeokolewa, umeokolewa. Kama Mungu akikuokoa usiku wa leo, akijua atakupoteza miaka kumi kuanzia leo hii, Yeye anavunja kusudi Lake Mwenyewe; asiye na kikomo, Mwenyezi, wa Milele, hekima ya milele, Mungu, hajui vya kutosha basi kujua kama wewe utashikilia ama kama hutashikilia. Basi, wakati anapokuokoa, unasema, “Vema, nitajaribu kumthibitisha. Nitaona atakachofanya,” basi Yeye hajui mwisho tokea mwanzo. Mungu anajua anachofanya, kamwe usiwe na wasiwasi juu ya jambo hilo. Ni wewe na mimi tunaoenda tukijikwaa-kwaa. Mungu anajua anachofanya. Naye alijua sisi...kama tungeweza kushikilia, ama kile tungalifanya.

<sup>297</sup> Sasa, Biblia ilisema ya kwamba, Esau na Yakobo, kabla hata mmoja wa hao watoto kuzaliwa, Mungu alisema, “Ninampenda mmoja, na namchukia huyo mwingine,” kabla

hata hawajapumua pumzi yao ya kwanza, kusudi uteule Wake ubakie kuwa ni wa kweli.

<sup>298</sup> Ibrahimu alikuwa ni nani? Tutamfikia mnamo dakika chache, hapa chini. Alikuwa ni nani, kwamba Mungu angemwita? Amwokoe bila ya chochote. Mungu hufanya agano na mwanadamu; mwanadamu huvunja agano lake. Lakini Mungu alifanya Agano hili na nafsi Yake, na kuapa kwa hilo, kwa nafsi Yake. Mwanadamu hana uhusiano wowote na jambo hilo. Ni kujua tangu zamani kwa Mungu Mwenyewe. Alifanya jambo hilo, hata hivyo.

<sup>299</sup> Sasa, unasema, “Vema, Ndugu Branham, basi kama nikiwa Mkristo, ninaweza kufanya tu jambo lolote nitakalo?” Kabisa. Kama wewe ni Mkristo, fanya lolote utakalo. Nami nitakuuhakikishia, hutakuwa na tamaa yoyote ya kufanya mabaya. Wewe fanya lolote. Mimi daima nilifanya yale tu niliyotaka kufanya. Na kama nikimtumikia Bwana kwa kuwa ninaogopa ninaenda jehanamu, simtumikii ipasavyo. Kama nikiishi mwaminifu kwa mke wangu kwa sababu ninahofu atanitaliki, mimi si mume mzuri sana. Lakini nisingemuumiza bila sababu, kwa kuwa ninampenda.

<sup>300</sup> Hivyo ndivyo ilivyo kwa Kristo, wakati mtu amezaliwa kwa Roho wa Mungu. Si kwa sababu alipiga makelele, alinena kwa lugha, ama mhemuko fulani; bali moyoni mwake, upendo uliingia na kupachukua mahali pa ulimwengu. Ninawaambia, anampenda Mungu. Anatembea pamoja Naye, kila siku. Haikubidi kumwambia mtu, “Si vizuri kufanya jambo hili, ama *lile*, ama *linginelo*.” Yeye anajua ni vibaya. Na, anatembea, yeye ni uzao mteule wa neema kuu ya Mungu. Kweli kabisa.

*Kwa maana haiwezekani hao waliokwisha kupewa  
nuru, . . . kukionja kipawa cha wito wa mbinguni, . . .*

Sasa, wakati mwingine tumeamini ya kwamba huyo alikuwa ni mtu ambaye alikwisha kupewa nuru na kuanguka tena, lakini Biblia haisomeki hivyo. “Haiwezekani kabisa kwa mtu,” anasema hapa, “ambaye amempokea Roho Mtakatifu, kuanguka wakati wowote.” Sasa lisome uone kama hilo si kweli. Angalia hapa, chukua kifungu hicho, kifungu kizima, na yaliyomo, muktadha, hasa.

<sup>301</sup> Sasa yeye anaanza kuzungumzia, ni kitu gani? “Na tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu.” Sasa, yeye alisema, “Si mambo ya kimwili, kuweka msingi hapa wa mafundisho na ubatizo na matengenezo, na kadhalika. Hebu na tusifanye hivyo. Na tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu.” Somo ni *utimilifu*, na utimilifu unatokana na Kristo. Nasi tuliiingiaje kwa Kristo? Kwa kuijunga na kanisa? “Kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja.” Sio kwa: kunena kumoja kwa lugha kulikonenwa; kumoja, kuingizwa kwa kupewa mkono; kumoja, kuingizwa kwa

kubatizwa kwa maji. "Bali kwa Roho mmoja tumebatizwa kuwa Mwili mmoja." Mnalipata? Huo ndio ukamilifu.

<sup>302</sup> Na wakati unapoingia ndani ya Huo, wewe uko ndani ya Kristo, na ulimwengu umekufa kwako. Nawe unatembea pamoja na Mwana-Kondoo kila siku, na hatua zako zinaongozwa na Mungu, jambo la kufanya. Loo, majaribio na mitihani tunayopitia! Unasema, "Je! wewe hujaribiwa?" Naam, bwana. Ni ninii...

<sup>303</sup> Neema ni vile Mungu alivyonitendea, kazi ni yale ninayomfanya Mungu. Sasa, wao watafanya mafundisho kutohana na jambo hilo, wanafikiri ya kwamba matendo ndiyo yanayokustahilisha. Kama ndivyo, basi si kipawa cha bure. Neema ni yale Mungu aliyokutendea. "Kwa neema mmeokolewa." Na matendo ni yale unayofanya kwa kuithamini hiyo neema aliyokuonyesha. Na kama unampenda, unapenda kufanya kazi za Bwana. Bila shaka, kwa maana, basi, wewe—wewe unampenda.

<sup>304</sup> Kumkubali Meda Broy, kama mke wangu, ndicho upendo ulichomfanya. Yale atendayo, kwa kuthamini: yeye ni mwanamke mwadilifu, anakaa nyumbani, anawatunza watoto, na anaishi maisha mazuri na ya uaminifu. Hiyo si kwa sababu hatujafunga ndoa; tumefunga ndoa. Bali yeye anafanya jambo hilo kwa kuthamini kwingi. Kama akizurura huko mjini, kila siku, na kuingia kwenye kila duka la hela kumi, na huku na huko mitaani, wala asioshe vyombo, wala chochote kile, tungali tumefunga ndoa. Kweli kabisa. Nilipoweka nadhiri yangu, tumeafikiana maneno. Yeye ni mke wangu. Mradi kuna uhai ndani yetu, yeye ni mke wangu. Hiyo ni nadhiri yake. Lakini jinsi anavyoonyesha shukrani kwa jambo hilo: anakaa nyumbani, na anawalea watoto, na kujitahidi kuwa mke mwaminifu.

<sup>305</sup> Ningeweza kutoroka na niwe siko nyumbani wakati wote, nikitangatanga tu kote nchini, na kumwacha karibu afe kwa njaa, ama chochote kile, niache watoto waishi bila kitu cha kula; tungali tumefunga ndoa. Hata kama akinaliki, ningali nimefunga ndoa, kadiri tu kuna uhai mwilini mwangu. Niliweka hiyo nadhiri, "Hata mauti yatakapotutenganisha." Hiyo ni kweli. Tungali tumefunga ndoa. Lakini, hata hivyo, mimi niwe ni mume ovyo kabisa. Yeye angekuwa ni mke ovyo. Kwa hiyo kama tunapendana, tunashikana na kukokota mzigo huo, pamoja.

<sup>306</sup> Hivyo ndivyo Mungu na Kanisa Lake alivyo, unapozaliwa katika Ufalme wa Mungu. Utakuwa na *heri* na *shari* zako, kweli, bali ungali u Mkristo, ungali umezaliwa na Roho wa Mungu. Mungu huenda akakuondoa duniani mapema.

... *haiwezekani kwa hao ambao waliokwisha kupewa nuru, na kukionja kipawa cha mbinguni,* . . .

. . . *hata wakaanguka baada ya hayo, haiwezekani kujifanya upya tena hata wakatubu;* . . .

<sup>307</sup> Sasa, ninajua mahali ambapo mnafikiria, kanisa. Hebu niwapeleke hatua moja kubwa zaidi, ili kwamba upande washika sheria upate kunyamazishwa kabisa. Hebu na twende katika Waebrania, mlango wa 10, na tuangalie jambo hili kwa muda kidogo tu.

<sup>308</sup> Mlango wa 10, kifungu cha 26.

*Maana, kama tukifanya dhambi kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi;*

*Bali kuna kuitazamia hukumu yenyе kutisha, . . . ukali wa moto ulio tayari kuwala wao wapingao.*

*Mtu aliyeidharau sheria ya Musa hufa pasipo huruma, kwa neno la mashahidi wawili au watatu.*

*Mwaonaje? Haikumpasa adhabu iliyo kubwa zaidi ingawa inapaswa . . . hata hivyo . . . kanyaga . . . mtu yule aliyeemkanyaga Mwana wa Mungu, na kuihesabu damu ya agano aliyotakaswa kwayo kuwa ni kitu ovyo, na kuifanyia jeuri kazi ya neema?*

<sup>309</sup> Sasa mnasema, “Na hilo je! Ndugu Branham? Hilo linaonekanaje?”

Sasa, kusoma tu, nafikiri, “Maandiko hayasemi hivyo.” Hayo hayaneni juu ya Mkristo. Hayo yananena juu ya mtu ambaye amelisikia Neno na kuliacha. Unaona?

*Maana, kama tukifanya dhambi . . . (Dhambi ni nini? Kutokuamini.) . . . kama tusipoamini kwa makusudi baada ya kuhubiriwa Injili, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi;*

<sup>310</sup> Dhambi ni nini? Kutokuamini. Soma Yohana Mtakatifu, mlango wa 4. Yesu alisema, “Yeye asiyeamini amekwisha kuhukumiwa.” Dhambi si kuvuta sigara, kunywa pombe, kufanya uzinzi. Unafanya jambo hilo kwa maana wewe si mwamini. Hayo ni matokeo yake tu. Unafanya hivyo kwa maana wewe ni asiyeamini. Kuacha tu kuvuta sigara, kuacha kunywa pombe, na kadhalika namna hiyo, hilo halimaanishi kwamba wewe ni—wewe ni Mkristo. Hayo ni matokeo tu ya kuongoka kwako. Lakini, unaweza, unaweza kufanya pande zote mbili, na ungali usiwe Mkristo.

<sup>311</sup> Sasa angalia.

  . . . yeye asiyeamini kusudi baada ya yeye . . .

<sup>312</sup> Si—si, “Baada ya kumpokea Kristo moyoni mwake.” Biblia haisema hivyo. Ilisema, “Yeye ambaye . . .”

  . . . kama tukifanya dhambi kusudi, tusiamini makusudi, baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, . . .

Mnalipata? Hakuwa akimzungumzia Mkristo, hata kidogo.

<sup>313</sup> Mwanamke fulani alinijia, si muda mrefu uliopita, na kusema, "Ndugu Branham, mimi ni Mkristo, lakini nilimkufuru Roho Mtakatifu."

<sup>314</sup> Nikasema, "Haiwezekani." Mkristo asingeweza kumkufuru Roho Mtakatifu. Huwezi kufanya hivyo. Roho ya Mkristo inashuhudia pamoja na Roho ya Kristo. Unaona? Nawe utaita, kila kitu cha Mungu, kwamba ni "cha Mungu."

<sup>315</sup> Lakini kama wewe una mawazo ya kimwili, utamdhihaki na kumcheka Roho Mtakatifu; sijali unaenda kanisani vipi, ungali ni mwenye dhambi, nawe unamkufuru Roho Mtakatifu. Walipomwona Yesu akitambua mawazo yao, walisema yeze alikuwa ni "mpiga ramli."

<sup>316</sup> Yesu alisema, "Mme-... Nitawasamehe kwa hilo, bali wakati Roho Mtakatifu atakapokuja, wewe sema neno moja dhidi Yake, hutasamehewa."

Kwa sababu, wao walisema, "Yeye ana roho mchafu," akimwita Roho wa Mungu, "kitu kichafu."

Mkristo hawezি kufanya hivyo. Mkristo daima ataita Roho wa Mungu, "Haki." Unaona? Mkristo hawezি kumkufuru Roho Mtakatifu. Ni mtu wa nje ambaye anakufuru.

<sup>317</sup> Hao hawakuwa ni Wakristo waliokuwa wanasmama pale. Ilikuwa ni watu wa kidini, ilikuwa ni Wayahudi wa kimapokeo, madakatari wa theolojia, na kadhalika, nao walikuwa wakimdhihaki Yeye pamoja na kazi Zake, wakiziita kazi za Mungu, ya kwamba, "Zilikuwa zikifanywa na roho mchafu."

<sup>318</sup> Na mnafikiri ni wangapi siku hizi wanamkufuru Roho Mtakatifu, walio na D.D.D., PhD. kwenye jina lao? Ni Waothodoksi washupavu mashuhuri wangapi, Wakatoliki, Waprotestanti, wanaotembea mitaani na kudhihaki matendo ya Roho Mtakatifu, kama vile tu wafanyakavyo wanachuoni hodari sana, nao ni wororo kama kifungo? Hiyo ni kweli. Lakini wanamdhihaki Roho Mtakatifu, na kwa hiyo wanamkufuru.

Lakini Mkristo aliyezaliwa mara ya pili hawezি kufanya jambo hilo. Yeye atasema, "Huyo ni ndugu yangu. Huyo ni Roho wa Mungu aliye hai." Hiyo ni kweli. Mkristo hawezি kumkufuru Roho Mtakatifu.

<sup>319</sup> Mwenye dhambi ndiye anayemkufuru Roho Mtakatifu; asiyeamini, *mwenye dhambi*, "asiyeamini." Kuna mambo mawili tu: ama wewe ni mwaminio, ama ni asiyeamini.

<sup>320</sup> Sasa, angalia hapa, kulimalizia hili kabisa sasa. Nilipata ono ambalo daima limenisumbua. Miaka mingi iliopita nilikuwa nikiangalia jambo hilo. Nilisema, "Loo, kama mtu akiisha kumpokea Roho Mtakatifu tu basi, na kisha angerudi nyuma, angepotea milele." Nisingeweza kufanya hili lingine kuafikiana na hilo.

<sup>321</sup> Nikasema, "Basi ni kwa nini kwamba Biblia ilisema, ya kwamba, 'Yeye ayasakiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye alienipeleka yuna Uzima wa Milele, wa Milele, wala hataingia kamwe hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani. Wote alionipa Baba watakuja Kwangu, wala hakuna atakayepotea, nitawafufua katika siku za mwisho. Hakuna mtu anayeweza kuwatoa mkononi Mwangu?" Hilo linaambatanaje na hili? Nisingeweza tu kufahamu jambo hilo, 'Haiwezekani kwa wale waliokwisha kupewa nuru.'" Niliwazia, "Kuna kasoro fulani. Siwezi kulielewa kabisa."

Basi nikaenda kuhudhuria mkutano mdogo wa Kipentekoste, miaka kadhaa iliyopita.

<sup>322</sup> Hakuna hata mmoja aliyesalia kanisani, nadhani, usiku wa leo, ambaye anakumbuka. Miaka mingi iliyopita, huu ulikuwa ni karibu na wakati maskani ilipojengwa. Isipokuwa, ingekuwa ni Ndugu Graham kule nyuma, ama mtu fulani. Sijui, ulikuwa hapa kwanza, ama hapana, ninyi ndugu. Ndugu Mahoney, nadhani, alikuwako. Naam, kabla tu sijaoa.

<sup>323</sup> Karama hiyo ikifanya kazi, nilikuwa nikiiogopa. Waliniambia yalikuwa ni mambo ya Ibilisi. Sikujua mpaka Malaika wa Bwana aliponiambia.

<sup>324</sup> Nilienda huko Mishawaka, nami nikaketi kwenye mkutano huo, na sijapata kamwe kusikia kupaza sauti kukuu hivyo na kulia na kumsifu Mungu. Nikawaza, "Ndugu, hapa ni Mbinguni." Na, loo, jinsi ambavyo wangerukaruka.

<sup>325</sup> Ilibidi waufanyie Kaskazini, kwa ajili ya ubaguzi. Watu weusi na wazungu walikuwa wako pamoja. P.A. ya W. na P.H.A.C. walikuwa kweli wameibuka na wakawa United Pentekoste. Lakini ni ufulufu wa jinsi gani waliokuwa nao, kule kwenye maskani ya Ndugu Rowe huko Mishawaka. Nami, jamaa kijana mdadisi, nikiwa nimeketi kwenye kiti cha nyuma, nilikuwa nikiangalia haya yote. Sijawahi kuona mambo haya hapo kabla.

<sup>326</sup> Kulikuwapo na mtu aliyekuwa ameketi hapa... Sijapata kuhadithia haya hadharani kabla ya hapo. Kulikuwapo na mtu aliyeketi upande mmoja, na mtu mwingine upande mwingine, na mmoja alinena kwa lugha, na huyo mwingine akaifasiri. Nao wangesema mambo mbalimbali yatakayotukia. Ndipo, *huyu* mmoja ananena kwa lugha, na *yule* anafasiri. Niliwazia, "Jamani, si ni jambo la ajabu hilo!" Nikawaza, "Ni tukufu jinsi gani! Hao hawana budi kuwa ni Malaika, wameshuka kwa mfano wa wanadamu."

<sup>327</sup> Vema, nilikuwa na dola moja na senti sabini na tano tu, za kwendea nyumbani, nami ni—ni—ningeweza tu kununua tangi moja la petroli. Nililala kwenye shamba la mahindi usiku ule. Nimeandika sehemu ya hayo katika kitabu fulani, bali si yote, maana sikutaka kuwaudhi. Na kwa hiyo, usiku huo, walisema,

“Wahubiri wote waje jukwaani.” Nilikuwa jukwaani. Nilikuwa mhubiri aliye kijana kuliko wote pale wakati huo.

<sup>328</sup> Kwa hiyo, kesho yake asubuhi, waliniomba nije nikahubiri. Nikajificha. Mwajua, yule mnegro alisema, “Huyu hapa.” Mnakumbuka hadithi hiyo, wakati aliponifichua nikiwa nimeketi pale.

<sup>329</sup> Na kwa hiyo baada ya kuhubiri siku ile, nikizungukazunguka, niliwazia “Laiti ningaliwapata hao watu wawili.” Waluongozza ule mukutano. Mmoja angeinuka na kugeuka kuwa mweupe usoni, angenena kwa lugha. Na huyo mwingine angeifasiri, na kutoa maneno, “BWANA ASEMA HIVI. “Kuna mtu *fulani* hapa, anaitwa *fulani wa fulani*, ambaye anapaswa kufanya *hivi na vile*.” Ndugu, ilikuwa ni kweli. Na huyo mwingine angeinuka na kunena kwa lugha, na angefasiri.

<sup>330</sup> Nikawazia, “Loo, jamani, hili si ni ajabu!” Kwa hiyo, siku hiyo, niliwazia, nilitoka nikaenda kuomba. Nikawaza, “Bwana, nifanyie jambo hilo tena.” Sikujuu niyaite nini, maono.

<sup>331</sup> Nilitoka nikaenda na kuomba, na nikamwomba Bwana anisaide. Nikazunguka jengo hilo, na ikatokea nilikutana na mmoja wao. Sasa, Bwana alinipa njia ya kujua mambo. Nilimpa mkono. Nikasema, “U hali gani?”

Akasema, “Sijambo? Jina lako ni nani?”

Nami nikasema, “Branham.”

“Loo,” akasema, “wewe ndiyeye yule kijana mdogo aliyehubiri asubuhi ya leo.”

Nikasema, “Naam, bwana.”

<sup>332</sup> Nilipokuwa nikizungumza naye, niliikamata roho yake. Naye alikuwa ni Mkristo halisi, ndugu Mkristo safi kabisa. Ninamaanisha, alikuwa ni mwaminio. Nikawazia, “Loo, hili si ni la ajabu!”

<sup>333</sup> Na yapata saa moja kutoka hapo, huko nje karibu na gari, ambalo lilikuwa limeelekezwa kwenye gari lingine kubwa mno, lilikuwa limeandikwa nyuma yake “Yesu Pekee”, na hapo nje alisimama yule mtu mwingine. Ndipo nikatoka nikaenda na kusema, “U hali gani, bwana?”

<sup>334</sup> Akasema, “Sijambo?” Kasema, “Wewe ni Ndugu Branham, aliyehubiri asubuhi ya leo.”

<sup>335</sup> Nikasema, “Naam, bwana, ndiyeye mimi.” Nikasema, “Aisee, ninafurahia hizo karama kuu za Mungu zinazofanya kazi ndani yenu ninyi ndugu wawili.”

<sup>336</sup> Akasema, “Asante, Bw. Branham.” Ndipo nikaanza kuhisi roho yake. Ono likatokea. Na kama nilipata kuzungumza na mnafiki, huyo hapo mmoja wao. Mkewe alikuwa ni mwanamke mwenye nyewe nyeusi, alikuwa akiishi na mwanamke mwenye

nywele za rangi ya shaba, alikuwa amezaa watoto wawili naye. Hakuwa Mkristo zaidi ya chochote kile ulimwenguni.

<sup>337</sup> Ndipo nikasema, “Nimeingia kwenye kitu gani? Nilidhani nilikuwa katikati ya Malaika, na sasa sina budi kuwa nipo katikati ya pepo. Jambo fulani limetukia. Hapa alikuwapo mmoja, Mkristo halisi; na Roho yeye yule anayeshuka juu ya mtu *huyu*, alikuwa akishuka juu ya mtu *huyu*.” Nikasema, “Sasa nimechanganyikiwa kabisa.” Sikujua la kufanya. Nililia na kusihi, kwa Bwana. Sikujua nikubali lipi.

<sup>338</sup> Walikuwa karibu kunifanya ni ninii... Akaniuliza kama nilikuwa “nimempokea Roho Mtakatifu?” huyu jamaa aliniuliza. Nikasema, “La, bwana, si vile mlivyompokea.”

Kasema, “Umewahi kunena kwa lugha?”

Nikasema, “La, bwana.”

Kasema, “Basi hujampokea.”

<sup>339</sup> Kwa hiyo nikasema, “Labda uko sahihi, ndugu yangu. Labda sjampokea, maana sina kile mlicho nacho.” Na baada ya kitambo kidogo, nilifurahi sikuwa na walichokuwa nacho.

<sup>340</sup> Kwa hiyo basi niliangalia jambo hilo, na nikaona jinsi lilivyokuwa likiendelea.

<sup>341</sup> Kwa hiyo, siku moja, nilikuwa nimetoka hapa njie nikiomba, muda mrefu uliopita. Nitawaambia ni kwa nini, yule niliyekuwa nikimwombea, ilikuwa ni Roy Davis. Nami nilikuwa hapa njie nikiomba, kwa maana alikuwa ameniita “kibaraka,” nami nilikuwa nikimwomba Mungu amsamehe kwa hilo. Naye alikuwa na mtambo wa kuchapisha vitabu mbali huko mpakani, alichapisha gazeti. Basi mtambo huo ukashika moto na kuteketetea, siku chache usiku baadaye, walipokuwa wakiutumia.

<sup>342</sup> Na kwa hiyo nilikuwa nimesimama mbali huko kwenye pango la kale nyuma ya Green’s Mill. Nilienda kule. Nami nilikuwa nikiomba, nilikuwa nimerudi kule, siku mbili. Niliweka Biblia yangu chini kwenye gogo la zamani, ambapo, nilimwonyesha Ndugu Wood, si muda mrefu uliopita, nikaweka Biblia yangu chini. Nikaketi kwenye hilo gogo kwa kutagaa. Ndipo upepo ukavuma. Nikawazia, “Imekuwa ni muda mrefu sana, nilikuwa kwenye hilo pango, ningesoma kidogo tu.” Kwa hiyo nikaichukua hiyo Biblia na kuanza kusoma, na huu ndio mlango uliokuwa umefunguliwa. Vema, nikaanza kusoma, ndipo nikaanza kushangaa basi. Unaona?

*Kwa maana hao waliokwisha kupewa nuru,...  
kukionja kipawa cha mbinguni, na kufanywa washirika  
wa Roho Mtakatifu,*

*...kulionja neno zuri la Mungu, na...zamani zijazo,*

*Wakaanguka baada ya hayo, haiwezekani kujifanya  
upya tena hata wakatubu; kwa kuwa wamsulibisha*

*Mwana wa Mungu mara ya pili kwa nafsi zao, na kumfedhehi kwa dhahiri.*

<sup>343</sup> Nikawazia, "Hayo hapo yale Maandiko." Lakini kitu fulani kilinishika. Ndipo nikaanza kuwazia, "Hapa ndipo alipozungumza huku nyuma, hapo mwanzo, 'Si kuweka msingi usio hai wa toba, hapo mwanzo. Si kuweka msingi wa toba,' na hapa anasema, 'Upya, kujifanya upya tena hata wakatubu. Bali tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu, tukiweka mambo haya huko nyuma.'" Ndipo nikaanza kusoma. Ndipo nikasoma kifungu kinachofuata.

*Maana nchi inayoinywa mvua inayoinyeshea mara kwa mara, na kuzaa mboga zenyen manufaa kwa hao ambaao kwa ajili yao yalimwa, hushiriki baraka zitokazo kwa Mungu;*

*Bali ikitoa miiba na magugu hukataliwa na kuwa karibu na laana; ambayo mwisho wake ni kuteketezwa.*

<sup>344</sup> Na niliposoma hilo, kitu Fulani kilinitikisa wakati huo huo. Ndipo nikawazia, "Bwana, hilo halimhusu Roy Davis. Kwa nini ufanye hivyo?"

<sup>345</sup> Nikaanza, nikafungua ukurasa mwingine. Ilibidi nilirudie, tena, "Haiwezekani kwa hao waliokwisha kupewa nuru," nikalipitia tena.

<sup>346</sup> Ndipo nikawazia, "Bwana, ni kitu gani hiki? Una maana gani, Bwana?"

<sup>347</sup> Ndipo nikageuka nikarudi pangoni mwangu, nipate kuliombea. Na nilipofanya hivyo, niliona dunia inazunguka. Na yote ilikuwa imelimwa, vizuri sana, dunia yote. Kisha nikamwona mtu aliyeavaa nguo nyeupe, akizunguka, alikuwa na kikapu mkononi mwake. Alikuwa akipanda mbegu alipokuwa akizunguka. Alienda akazunguka kwenye mpindiko wa dunia. Na mara alipoenda upande wa pili, huyu hapo jamaa fulani anakuja amevaa nguo nyeusi sana, jamaa anayeonekana ni mjanja sana, akinyemelea namna *hii*, akiangalia. Naye alikuwa na mbegu. Naye alikuwa akitupa kitu fulani nyuma yake, alipokuwa akiizunguka dunia; akimwangalia kila mtu na kutupa. Nilisimama na kuangalia hilo ono.

<sup>348</sup> Baada ya yeche kuondoka, dunia ilizunguka, na kulikuwako na zao zuri mno, nalo lilikuwa ni la ngano. Na kulikuwako na magugu, makwekwe na mambo kadha wa kadha katika hiyo ngano.

<sup>349</sup> Ukame ukatokea. Na, loo, jinsi ambavyo maskini ngano hiyo ndogo ilivyoinamisha maskini kichwa chake kidogo, na ilikuwa na kiu ya maji. Maskini kwekwe lilikuwa limeinamisha kichwa chake, na lilikuwa na kiu ya maji. Kila mtu alikuwa akiomba mvua. Na baada ya kitambo kidogo, hili hapa wingu kubwa likaja na kuimwagilia kabisa dunia nzima maji. Ndipo

maskini kwekwe likaruka, likaanza kupaaaza sauti, "Utukufu kwa Mungu! Haleluya! Bwana asifiwe!"

<sup>350</sup> Na maskini hiyo ngano ndogo, iliruka, ikaanza kupaaaza sauti, "Utukufu kwa Mungu! Bwana asifiwe!"

<sup>351</sup> Na ndipo Maandiko yakanijia, ambayo yanapatikana katika Kitabu cha Mathayo, mlango wa 5 na kifungu cha 45. Basi sikilizeni yale Yesu aliyosema, katika Mathayo 5:45. Basi sikilizeni kwa makini sasa tunaposoma. Mathayo, mlango wa 5 na kifungu cha 45, 46; kuanzia cha 44.

*Lakini mimi nawaambia, Wapendeni adui zenu,  
wabarikini wanaowalaani, na mwatendee mema  
wanaowachukia, waombeeni wanaowatumia vibaya,  
na wanaowaudhi,*

*Ili mpate kuwa...kuitwa...ninyi ili mpate kuwa  
wana wa Baba yenu aliye mbinguni; maana yeye  
huwaangazia jua lake waovu na wema, huwanyeshea  
mvua wenye haki na wasio haki.*

<sup>352</sup> Kwa hiyo, unaona, mvua ile ile inayofanya ngano kukua, inalifanya gugu kukua. Na, kwa hiyo, nilipata hiyo picha. Huyo hapo shahidi wako wa kimwili, aliye mumo humo kanisani. Lakini matunda yake... Huenda akapaaza sauti, akaruka, akacheza, akanena kwa lugha; bali matunda yake: yeye ni kwekwe. Kisha kuna yule mwingine, ambaye ana Roho yeye yule. Roho Mtakatifu anawenza kushuka moja kwa moja katika kundi la watu, na mnafiki anawenza kupaaaza sauti, kwa Roho Mtakatifu huyo, kama tu vile kwekwe linavyoweza kuishi kwa mvua iliyotumwa. Hayo ndiyo Paulo anayonena habari zake hapa. Lakini haiwezekani kwa kwekwe kufanyika ngano, wala ngano kufanyika gugu. Mnalipata? [Kusanyiko linasema, "Amina." —Mh.]

*Kwa maana hao ambaao tayari wamepewa nuru, na  
kukionja kipawa cha mbinguni, na kufanywa washirika  
wa kipawa cha Roho Mtakatifu,*

*Na kilionja neno zuri la Mungu, na nguvu za  
ulimwengu ujao,*

*Wakaanguka baada ya hayo, haiwezekani kuwafanya  
upya tena...*

Sikilizeni yale aliyosema.

*Maana nchi inayoinywa mvua inayoinyeshea dunia  
mara kwa mara,... na kuilima hapa, na kuitayarisha;*

*Bali ikitoa miiba na magugu hukataliwa na kuwa  
karibu na laana;...*

*Sasa, kwa sababu hiyo, tukiacha kuyanena  
mafundisho ya kwanza ya Kristo, tukaze mwendo ili  
tuufikilie utimilifu; tusiweke msingi tena wa kuzitubia*

*kazi zisizo na uhai, . . . kwa Mungu, na kwa imani, na kadhalika.*

Na wa mafundisho ya mabatizo, . . . kuwekea *mikono*,  
na kadhalika; . . .

<sup>353</sup> Unaona, mwamini wa kimwili, huko zamani katika siku hiso, kama tu vile ilivyo siku hizi, anapenda kusema, “Vema, mimi ni mfuasi wa kanisa. Nimetubu. Ni—nimekuja, nilikiri. Nimebatizwa.” Unaona, wanategemea hayo matengenezo ya kimwili. Nayu yanafanya nini? Yanaza makwekwe.

<sup>354</sup> Utimilifu unafanya nini? Ndio ngano. Ngano ni Neno la Mungu. Yeye anaitumia kama Neno Lake. Ni Mbegu. Inazaa.

<sup>355</sup> Inategemea ni mbegu gani iliyopandwa moyoni mwako. Kama ukija kanisani kwa sababu tu unaogopa jehanamu, kama ukijiunga na kanisa kwa sababu hutaki—hutaki kwenda jehanamu, wewe ungali ni kwekwe. Kama u—kama ukijiunga na kanisa kusudi upate kupendwa sana na watu, wewe ungali ni kwekwe. Kama umefanya mambo haya yote ya kidesturi ambayo yanapaswa kufanywa, na hayo tu ndiyo uliyo nayo, wewe ungali ni kwekwe.

<sup>356</sup> Lakini Mkristo halisi na wa kweli hukaza mwendo ili aufikilie utimilifu mpaka ulimwengu umekufa nawe unakuwa kiumbe kipywa katika Kristo Yesu. Ndipo, haiwezekani kwa mtu huyo kuanguka kamwe. Ndivyo Biblia ilivyosema! Unaona jinsi jambo hilo linavyolingana na Maandiko mengine? Unaona jinsi yanavyoliingiza mle ndani sawasawa kuliweka mahali pake?

<sup>357</sup> Inawezaje kusema hapa, “Mtu ambaye amekwisha kuokoka hawezi kupotea kamwe” kisha ije hapa na iseme, “Lakini, kama umepotea, ama ukikufuru, haiwezekani”? Hakika, kama wewe ni anayekufuru, wewe si Mkristo.

<sup>358</sup> “Hakuna mtu, anenaye kwa Roho wa Mungu, asemaye, Yesu amelaaniwa.” Yohana Mtakatifu 4 . . . ama Yohana wa Kwanza 4. Hakuna mtu anayenena kwa Roho wa Kristo, asemaye, Yesu “amelaaniwa.” Kila roho, ya Mungu, iliyoko katika Kanisa la Kikristo, inakubaliana na kila kitu alichosema Mungu.

<sup>359</sup> Tunasoma hapa, na kusema, “Alijeruhiwa kwa makosa yetu. Kwa mapigo Yake sisi tunaponywa.”

<sup>360</sup> Maskini mtu mwenye mawazo mabaya ya kimwili anasema, “Siku za miujiza zimepita. Mimi ni Dk. Jones.” Unaona? “Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu. Hakuna kitu kama dini ya kutoka moyoni. Ninyi ni kundi tu lililochochewa. Mna mhemuko. Mnaona, ni hayo tu. Hamna lolote. Sisi ni Wapresbiteri. Sisi ni Walutheri,” ama chochote kile. “Tunajua tunaposimama.”

<sup>361</sup> Lakini Roho wa Mungu anasema nini? Yesu Kristo, yeye yule hapa! “Amina,” asema Roho wa Mungu. Anakubaliana

upesi na Neno. Naam, bwana. Liko pale pale. Unaona ninalomaanisha sasa?

<sup>362</sup> “Matengenezo haya ya kimwili husababisha mauti,” alisema Paulo.

<sup>363</sup> Lakini mahali Uzima umekuja, utimilifu huu, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, anayemwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele, wala hataingia hukumuni, bali amepita toka mautini kuingia Uzimani. Nitampa Uzima wa milele, nitamfufua katika siku za mwisho. Wote alionipa Baba watakuja Kwangu Mimi, wala hakuna mmoja wao amepotea.” Haiwezekani apotee.

<sup>364</sup> Kwa hiyo, hivi ndivyo linavyofanya—linavyofanya. Watu wanafikiri ya kwamba eti linawafanya watu wawe wazembe. Ndugu, humtumikii Mungu shingo upande. Mungu si mmoja wa hawa jamaa walio na kiboko cha ngozi ya nyoka mweusi, akikusukuma-sukuma. Yeye ni Baba. Yeye ni Upendo. Mungu ni Upendo. Na Biblia ilisema, katika Yohana Mtakatifu, “Yeye apendaye ni wa Mungu.”

<sup>365</sup> Unampenda Mungu. Nisingehofu, kama nilitoka nikaenda na—na nikalewa usiku wa leo. Sijapata kunywa pombe kamwe, maishani mwangu. Lakini kama ningalitoka niende na nikalewe, nisingeogopa kupigwa mijeledi. Hiyo siyo sababu siendi—siendi, siendi kufanya jambo hilo. Sababu ya mimi kutofanya jambo hilo, ni kwa sababu ninampenda. Yeye ananipenda. Si matendo ya sheria. Si jambo fulani ambalo ninapaswa kufanya. Ni kwa sababu Yeye tayari amenifanya jambo fulani, nami ninampenda kwa ajili ya jambo hilo. Haya basi.

<sup>366</sup> Kwa hiyo, huyo Roho akiwa hapo ndani, ambaye ameahidiwa, “Ninampa Uzima wa milele, wala kamwe hawataangamia.” Je! Yeye alisema uongo ama alisema Kweli? Alisema Kweli. Kwa hiyo, unaona jinsi jambo Hili linavyofasiriwa? Kutewezeckana ni kwa mtu kuanguka akiisha kuja katika neema. Hawezi. Anaweza kuanguka, hakika, bali si kurudi kutubu, kurudi mahali hapo na kufanya matendo ya kale tena.

<sup>367</sup> Kwa hiyo, ninyi nyote mnaokimbia-kimbia toka ufufuo mmoja hadi mwингine, mahali pamoja na kisha pengine, hivi hamwoni kwamba ninyi hamko thabit? Hamjaimarishwa. Sasa, hakika... Mnasema, “Ndugu Branham, sijui kama...” Hakika Mungu asingenipa huduma aliyonipa, kisha aniache niwe makosani. Na kama haingethibitishwa kwa Maandiko, basi ingekosea, lakini haya hapa Maandiko ya kuiunga mkono.

<sup>368</sup> Makanisa kamwe hayakukosa mahali... Watu wanaenda, wanajiunga na kanisa, wanazozana, wanapigana, wanabishana, na—na kila kitu, na wanaishi tu kila namna ya maisha ya kimwili, “Loo, ndiyo, mimi ni Mkristo.”

<sup>369</sup> Nilisikia ushuhuda fulani leo wa maskini mama mmoja aliyeniambia ya kwamba mumewe alikuwa akizurura na mwanamume fulani. Amewashika, mahali baada ya mahali. Na huyo mwanamke anasema, “Nitakujulisha, ‘Mimi ni Mkristo.’”

<sup>370</sup> Mwangalie hapa Jimmy Osborne, huku nje akihubiri Jumapili asubuhi; na kucheza bugi-bugi, roki na kila kitu, juma zima.

<sup>371</sup> Mwangalie Elvis Presley, mtindo wa mwaka wa 1947 wa Yuda Iskariote, anajiunga na Assemblies of God, Mpentekoste, akinena kwa lugha kwa ajili ya Roho Mtakatifu, na amepeleka watu wengi zaidi kuzimu kuliko vilabu vyote vya pombe ambavyo vimekuwako katika muda wa miaka hamsini iliopita. Amezipotosha akili za watoto matineja kote ulimwenguni, mpaka wasichana wadogo wanavua nguo zao za ndani na kuzitupa jukwaani, naye aziandike jina lake. Mchafu sana hata hawatamwonyesha kwenye televisheni, kutoka kiunoni kwenda chini, jinsi mwili wake ulivyokaa. Ati Roho Mtakatifu, kunena kwa lugha, kuwa ni thibitisho? Loo, ndugu, kama Roho Mtakatifu angalikuwapo pale, asingelitenda jinsi hiyo. Wewe una akili nzuri ya kupambanua mambo hayo. La hasha. Mungu anapenda usafi na utakaso na utakatifu.

<sup>372</sup> Sijifanyi msafi na asiye na taka na mtakatifu nipate kujifanya Mkristo. Lakini Kristo, ndani yangu, anayaishi hayo ndani yangu. Nami ninampenda. Na kama nikifanya jambo lolote baya, linanihukumu, papo hapo. Ninasema, “Mungu, nisamehe.” Kila siku, sina budi kuomba msamaha, kila siku. Nawe unafanya hivyo, pia. Hakika, unaomba msamaha.

<sup>373</sup> Lakini sasa kama wewe ni—kama wewe ni wa kimwili, unangojea tu huko nyuma, unasema, “Aa, vema, hilo ni sawa, mimi ni mfuasi wa kanisa.” Unaona? Na wakati unapokufuru, ndipo huwa huna ile Imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja. Ndipo unaidhihaki Hiyo, na kuiita, “Pepo mchafu.” Unasema, “Hilo ni kundi la watakatifu wanaojifingirisha.” Ndipo, unajitenga wewe mwenyewe kati ya neema na hukumu, ndipo basi umekwisha milele.

<sup>374</sup> Yesu alisema, “Neno moja dhidi Yake, halitasamehewa kamwe katika ulimwengu huu wala ulimwengu ujao.” Na Mkristo, aliyezaliwa kwa Roho, hawezi kusema maovu juu ya Huyo, maana hawezi. Anakubaliana Naye. Hiyo ni kweli.

<sup>375</sup> Hiyo ndiyo sababu watu wanajaribu kuniambia, hiyo Nguzo ya Moto hapo, inayotokea hapa pamoja nasi, wanajaribu kusema, ya kwamba, “Hiyo ilikuwa ni Ibilisi,” ya kwamba, “Ilikuwa tu ni hadithi za kujibunia,” yote haya. Lakini kamera ilithibitisha ya kwamba haikuwa ni hadithi. Na kazi hizo zimo moja kwa moja kwenye Biblia hasa, Nguzo ile ile ya Moto iliyokutana na Paulo alipokuwa akienda zake Dameski. Mambo

haya yote aliyofanya kule nyuma, anafanya hayo vile vile kabisa, kwa Biblia. Yeye ni Kristo, Mwana wa Mungu.

<sup>376</sup> Na wakati tunapozaliwa mara ya pili, tuna Uzima wa milele, wala hatuwezi kuangamia. Isingewezekana kwa mtu kuanguka. Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema.

<sup>377</sup> Sasa, sikiliza, angalia yale asemayo Paulo. Nitasoma mengine yote, na tuone kama hilo halisikiki sawa, sasa. Hebu na tuendelee, kwa dakika moja tu. Kifungu cha 8.

*Bali ikitoa miiba na magugu hukataliwa na kuwa  
karibu na laana; ambayo mwisho wake ni kuteketezwa.*

(Huyo ni yule asiyeamini.)

<sup>378</sup> Sasa mwangalie Paulo. "Lakini, wapenzi, . . ." Sasa yeye anazungumza juu ya hao kujaribu kurudi chini ya torati, mwajua, kujaribu kufanya matendo yote ya torati, hata hivyo wao ni wa kawaida tu za dini wavezavyo kuwa. Wana mabatizo na kuwekea mikono, na mambo haya yote.

*Lakini, wapenzi, . . . katika habari zenu tumesadiki  
mambo yaliyo mazuri zaidi, . . .*

Haya basi. Msikilize sasa.

*. . . na yaliyo na wokovu. Ijapokuwa—ijapokuwa—  
ijapokuwa katika hili twanena hayo.*

*Maana Mungu si dhalimu hata azisahau kazi zenu,  
na bidii yenu ya pendo lile mlilolidhihirisha kwa jina  
lake, kwa kuwa mmewahudumia watakatifu, na hata  
hivi sasa mngali mkiwahudumia.*

<sup>379</sup> Mnaona yale anayonena habari zake? Yeye haneni juu ya Wakristo kuanguka, kutowezezana kufanywa upya. Yeye ananena juu ya waamini wa kimwili amba wanapitia katika matengenezo ya kawaida. "Lakini," yeye alisema, "kweni ninyi mliokuwa mmekwisha kuzaliwa mara ya pili, ninyi amba ni Wakristo, wapenzi, katika habari zenu tumesadiki mambo yaliyo mazuri zaidi. Hamsemi mambo hayo. Hamwishi maisha ya aina hiyo. Ninyi ni salama katika Kristo."

Yeye alisema nini huku nyuma? Sasa hebu na twende kwenye Waebrania 10, mahali tulipokuwa asubuhi ya leo, tena. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

<sup>380</sup> Sasa hebu na tugeukie tena basi, tena, katika Waefeso 4:30. Na hebu tuangalie jambo hili, kwa dakika moja tu, na tuone vile hili linavyosema, kuunga jambo hili mkono, kufanya Andiko liambatane na Andiko. Waefeso 4, hebu tuone. Waefeso 4:30. Hebu na tusome tuone inavyosema. Sikilizeni.

*. . . msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa  
Mungu, . . .*

Aa? Tunabatzwaje kuwa katika huo Mwili? Roho mmoja.

*...msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu; ambaye kwa yeye mlitiwa muhuri mpaka siku ya ukombozi wenu.*

Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mmetiwa muhuri kuwa katika Mwili wa Kristo, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, si kutoka ufufuo mmoja hadi mwininge, bali mpaka Siku ya mwili wa ukombozi. Hivyo ndivyo mlivyo. Kwa hiyo, hakuna njia kwako kupotea.

<sup>381</sup> Unaogopa. Na hiyo ndiyo sababu kuogopa, kuogopa, hofu huambatana na shaka.

Upendo huambatana na imani. Ninampenda Baba yangu. Mimi simwogopi, maana ninampenda. Asingeweza kunidhuru. Atanitendea mema. Kama ningemwogopa, na, “Loo, sijui kama Yeye atafanya jambo hilo, ama hatalifanya.” Unaona?

<sup>382</sup> Lakini kama ninampenda, “Ndiyo, Baba, ni—ninakupenda. Na mimi ninajua ya kwamba Wewe—Wewe ni Baba yangu, na unanipenda, wala siogopi ila kwamba utatimiza Neno Lako. Ni ahadi Yako kwangu.” Hivyo ndivyo Roho wa Mungu anavyofanya.

<sup>383</sup> “Lakini, loo, kama ningalifanya jambo *hili*, kama ningalifanya *lile*.” Unaona, hapo unakuja upande wa kisheria, tena. Kamwe usiende upande wa sheria. Ni kivuli.

<sup>384</sup> Upande ulio halisi ndio mtu unaotaka. Tayari ni kazi iliyomalizika. Kristo alikufa, nayo dhambi iliuawa wakati alipokufa. Na kama Mungu alikuchagua tangu zามانى kwa ajili ya Uzima wa Milele, “Wote alionipa Baba, watakuja Kwangu.” Haya basi, huwezi kupotea. Wewe uko salama milele. “Kwa kuwa kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja, na kwa dhabihu moja Yeye amekamilisha milele.” Haya basi. Hakuna njia ya sisi kupoteza. Kweli. Sasa, hivi hilo halikufanyi kujisikia vizuri? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

<sup>385</sup> Sasa, wewe unajuaje u Mkristo? Wakati roho yako inaposhuhudia na Roho Wake, wakati upendo wa Mungu umo moyoni mwako, wakati ukiwa una upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, subira, wema, upole. Hapo ndipo wewe . . . Matunda ya Roho yanayafuata maisha yako.

<sup>386</sup> Si kwa sababu unaweza kucheza katika Roho, loo, kwa mdundo huu wa kisasa, kufanya shamrashamra za piano, kwa kucheza huku kwangi katika Roho. Mambo hayo yote ni sawa. Bali walichukua jambo lote zima huko kwenye upande wa sheria, unaona, na kwa hiyo, walimwacha Roho wa Mungu huko nyuma.

<sup>387</sup> Hiyo ndiyo sababu, wakati Mungu alipoanza kujidhihirisha Mwenyewe, walisema, “Uppuuzi. Hatutaki kuwa na uhusiano wowote na jambo Hilo.” Hawamjui Mungu. Hawajamwona. Hawawezi kumfahamu, kwa maana kuna uhai wa tofauti mle

ndani. Yeye hajui... Kwekwe halijui yale ngano inayofanya. Yeye ni uhai wa tofauti.

<sup>388</sup> Hivyo ndivyo ilivyo kwa Mkristo, kwa mwamini wa kimwili, anayedai, anayetoka akaenda na kudai, "Loo, ndiyo, mimi ni Mkristo." Msokoto mkubwa kinywani mwake, kama maksai wa Texas aliyeng'olewa pembe.

<sup>389</sup> Mwanamke aliyeavaa kaptura yake, anasema, "Loo, ndio, mimi ni mfuasi wa kanisa. Hakika, mimi ni mfuasi wa kanisa." Matunda yako yanathibitisha ya kwamba wewe si kitu ila ni mtu wa kimwili. Hiyo ni kweli. Hakika, ni kweli. Kuna kitu kimoja tu cha kuelezea sababu ya jambo hilo: hilo ni ama upungufu wa akili ama ni roho ya ukware juu yako. Hiyo ni kweli.

<sup>390</sup> Kama unataka kufanya kama ulimwengu, Biblia ilisema, "Ukiipenda dunia ama mambo yaliyo katika dunia, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako." Kwa hiyo hivyo ndivyo ilivyo.

<sup>391</sup> Sasa, unasema, "Loo, Biblia ilisema, basi inanipasa kufanya hivyo." La, siyo hivyo. Kaa hapa mpaka Kristo amekufanyia jambo fulani, ambacho kinatoa hayo ndani yako. Ndipo umezaliwa kwa Roho wa Mungu. Si yale unayofanya, ni yale Yeye aliyokufanyia. Mpaka utakapopata upendo ya kwamba umepita toka mautini kuingia Uzimani. Na ndipo uyaangalie maisha yako, kama yana—kama yanalingana. Si kwa sababu eti unajaribu kuyaumba maisha yako, bali ni kwa sababu Mungu anakutiisha kwa Roho Wake. Si wewe ujiongozaye mwenyewe katika njia ya Mungu. Ni Mungu akikuongoza katika Njia Yake Mwenyewe. Si wewe uongozaye, bali ni Mungu aongozaye.

<sup>392</sup> Sasa angalia jambo hili, sasa, wakati tu tukielekea kufikia mwisho. Kifungu cha 11.

*Nasi twataka sana kila mmoja wenu aidhihirishe bidii  
ile ile, kwa utimilifu wa matumaini hata mwisho;*

*Ili msiwe wavivu, bali mkawe wafuasi wa hao  
wazirithio ahadi kwa imani na uvumilivu.*

<sup>393</sup> Sasa, tamshi moja tu zaidi hapa.

*Kwa maana Mungu, alipompa Ibrahimu ahadi, kwa  
sababu alikuwa hana mkubwa kuliko yeye mwenyewe  
wa kumwapa, aliapa kwa nafsi yake.*

*Akisema, Hakika yangu kubariki nitakubariki, na  
kuongeza nitakuongeza.*

<sup>394</sup> Wakati Mungu alipokutana na Ibrahimu! Sasa, Ibrahimu alilipokea lile agano, pasipo ustahili wowote kabisa. Lile agano ilifanywa kwa Ibrahimu. Ni neema kamili, kwa jumla. Ibrahimu hakuwa ni mtu bora zaidi. Hakuwa mtu wa utakatifu. Yeye alikuwa ni mtu wa kawaida tu. Naye Mungu, kwa kuteua, alimchagua Ibrahimu kwa sababu Mungu alimteua; si kwa sababu Ibrahimu alilitaka jambo hilo, ati kwa sababu Ibrahimu alifanya hivi, kwa sababu alikuwa ni mtu mzuri, sababu alikuwa

na ustahilifu wowote. Bali lilikuwa ni chaguo la Mungu. Mungu alimchukua Ibrahimu.

<sup>395</sup> Leo, kama nilivyosema, ninaamini, “Tunawachagua wahubiri wetu.” Tunazunguka, tukisema, “Vema, mmoja wa mashemasi aliondoka. Hebu na tumtafute mtu anayefaa sana humu jengoni kupachukua mahali pake. Vema, mchungaji aliondoka; na tutafute, tumpate aliye bora sana.” Mara nyine hilo si sawa.

<sup>396</sup> Wakati walipomchagua mtu fulani kupachukua mahali pa Yuda, walimpata mtu asiyefaa. Walimpata mwungwana, Mathiya, mwandishi mashuhuri, msomi, mwanadiplomasia. Walisema, “Yeye atafaa kabisa kwenye nafasi hiyo. Da! anaonekana kama mtu anayefaa hasa.” Bali halikuwa ni chaguo la Mungu. Ndipo akamchukua mtu huyu, naye hajawahi kumfanyia Mungu lolote.

<sup>397</sup> Lakini Mungu alichukua chaguo la maskini Myahudi mdogo mwenye hasira kali mwenye pua kama ndoano aliyeshuka kuja kule. Uso wake, wote, “Nitashuka niende huko. Nitawakamata.”

<sup>398</sup> Mungu akasema, “Ninaona kitu fulani ndani yake. Nitamtumia.”

<sup>399</sup> Ndipo Mungu akamtokea, ile Nuru kubwa pale. Naye akasema, “U nani Wewe, Bwana?”

<sup>400</sup> Kasema, “Mimi ni Yesu. Mbona, ni vigumu kwako kuupiga teke mchokoo. Mbona unaniudhi?” Namna hiyo, ndipo Mungu akamchukua mtu *huyo* na kumfanya mmoja wa watu mashuhuri sana walipata kuwasili kwenye uso wa dunia tangu Yesu Kristo. Hilo lilikuwa ni chaguo la Mungu.

<sup>401</sup> Siku hizi, tunajaribu kujichagulia. Ninyi makanisa, mnamtuma mtu *huyo* hapa, na mtu *yule* hapa. Haipaswi kufanywa namna hiyo. Mungu ndiye anayeongoza. Ni Mungu ndani ya mambo yote, katika yote, juu ya wote; si vile vinavyoongoza baadhi ya vitabu vyatka kanisa fulani. Ni yale Mungu aliyosema juu ya jambo fulani, ndiyo yanayoleta tofauti.

<sup>402</sup> Angalia. Mungu alimpa Ibrahimu ahadi, isiyo na masharti. Na sasa, hebu ngoja, haikumpasa Ibrahimu kufanya kitu chochote. Mungu alisema, “Nimefanya hivyo tayari.”

<sup>403</sup> Mungu alimpa Adamu ahadi, kasema, “Adamu, kama hutagusaa *hili*, utaishi milele. Lakini siku utakayokula *hili*, siku hiyo utakufa.”

<sup>404</sup> Adamu alisema, “Nashangaa kabisa, hata hivyo, hiki ni kitu gani?” Yeye anatoka kwenda na kulila, akichezacheza nalo.

<sup>405</sup> Kila wakati Mungu akifanya...mwanadamu afanyapo agano lake na Mungu, ama Mungu na mwanadamu, mwanadamu anavunja sehemu yake. Kwa hiyo ilibidi Mungu afanye jambo fulani, kwa kuwa alikuwa ameona kile mwanadamu alichokuwa. Nao walikusudiwa tangu zamani, walikuwa wameteuliwa, basi

ilibidi Mungu afanye jambo fulani. Kwa hiyo Mungu alishuka akaja na kufanya agano Lake na Ibrahimu, bila masharti. Kama lisingekuwa lisilo na masharti, Ibrahimu angalipotea, siku nyingi.

<sup>406</sup> Mwangalie akiwa ameketi kule Gerari, amerudi nyuma, akisema uongo. Kisha akamtoa mke wake kwa mwanamume mwingine, apate kujiokoa uhai wake. Ni mwanamume wa namna gani! Ameketi kule, na huku amerudi nyuma. Mungu alimwambia, alisema, “Usiondoke hapa. Kaa hapa.” Njaa ilimfukuza. Alitangatanga akaenda ambako mambo yalikuwa ni afadhali. Mnajua yanayompata mtu wakati anapoendea ile njia iliyo rahisi.

<sup>407</sup> Alitangatanga huku na huko, sehemu zile ambako nyasi zilikuwa ni za kijanikibichi zaidi. Ndipo aliposhuka akaenda kule, akamwambia huyo mfalme ya kwamba mke wake alikuwa ni “dada” yake, apate kuyaokoa maisha yake. Sasa, huo ulikuwa ni uongo. Na mwanamume yejote, ambaye angemchukua mke wake na kumtoa kwa mwanamume mwingine, apate kuoko maisha yake! Huyo hapo, ameketi kule kwenye hema dogo, mtu aliyerudi nyuma, akisema uongo, na ametoka moja kwa moja kwenye ninii, amekatiliwa mbali na ile ahadi na kila kitu, bali alikuwa angali ni nabii wa Mungu.

<sup>408</sup> Na huyo hapo Abimeleki, alikuwa ni mtu mzuri wa utakatifu. Hakika, alisema sala zake kila usiku. Akamwona huyu bibi kizee, wa umri wa miaka mia moja, amewasili kule, mzuri na ni msichana tena. Akasema, “Huyo ndiye msichana ambaye nimekuwa nikimngojea, kwa hiyo nitamwoa tu.”

<sup>409</sup> Ibrahimu akasema, “Unaweza kumchukua. Yeye ni dada yangu.”

Yeye mke naye, “Huyo ni ndugu yangu.”

<sup>410</sup> Kwa hiyo anamchukua anampeleka kule na kuwaagiza wanawake wamwogeshe vizuri na—na kumvalisha nguo nzuri, na kumremba kama bi—binti mfalme. Ndipo akasema sala zake, akajilaza kitandani, kisha akainua miguu yake juu, na kusema, “Kesho, nitamwoa yule msichana mrembo wa Kiebrania, yule—yule dada wa yule mvulana aliye kule. Loo, itakuwa safi sana. Ee Bwana, unajua jinsi ninavyokupenda! Naam, bwana. Ni ajabu sana!”

<sup>411</sup> Ndipo Mungu akasema, “Wewe ni kama tu mtu aliyekufa.” Aa!

[Ndugu Branham anakohoa—Mh.] Samahani. Ibra- . . .

<sup>412</sup> Mbona, Ibrahimu alikuwa ameketi pale, mwongo, na amekengeuka. Na hapa alikuwapo mtu huyu, mtu mkweli na mnyofu na mwaminifu. “Mbona,” akasema, “Bwana, Unajua unyofu wa moyo wangu. Yeye si aliniambia, huyo alikuwa ni ‘dada’ yake?”

<sup>413</sup> Kasema, “Ninajua unyofu wa moyo wako. Hiyo ndiyo sababu ninakuzuia usinitende dhambi. Hiyo ni kweli. Ninajua unyofu wa moyo wako. Bali mume wake ni nabii Wangu.” Haleluya! Loo, kama hiyo si neema, ni kitu gani? “Amerudi nyuma, anasema uongo, na ameketi kule, bali huyo angali ni nabii Wangu. Chukua dhabihu, na umwendee, na umrudishe mkewe, la sivyo, wewe ni maiti. Sitasikia sala zako tena. Mwambie akuombee.” Amina. Haya basi. “Huyo ni nabii Wangu.”

Sasa, unasema, “Loo, laiti ningalikuwa Ibrahimu.”

<sup>414</sup> “Tukiwa wafu katika Kristo, sisi ni Uzao wa Ibrahimu, nasi tu warithi kulingana na ile ahadi.” Kweli. Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema. Mngetaka kulisoma Hilo? Mbona, Biblia ilisema hilo, ya kwamba hiyo ahadi haikuwa ni ya Ibrahimu peke yake pia na wazao wake. Kama vile wewe, Ibrahimu alikuwa na kwa wazao wengi, hakika, watoto wengi. Ishmaeli alikuwa ni mtoto wake. Alikuwa na watoto saba ama nane baada ya Sara kufa, kwa mwagine, Ketura. Lakini, angalia, huo uzao ulikuwa ni ule ulioahidiwa, ambao ulikuwa ni Isaka, na kwa kupitia Isaka akaja Kristo, kupitia kwa Kristo tukaja sisi. Ahadi hiyo haina masharti.

<sup>415</sup> Sasa, vipi kuhusu Ibrahimu? Mbona, ingekuwa ndio hatima yake, isingwezekana kwake kurudi tena. Hakika. Isingwezekana kwa Sauli kurudi tena kabisa, kama hivyo ndivyo ilivyo, ingekubidi uyasome Maandiko namna hiyo. Unaona? Lakini haikuwa hivyo. Ahadi ya Mungu inadumu milele.

<sup>416</sup> Hebu na tusome hapa kwa dakika moja tu. Ninataka mpasome. Ninataka mfungue Wagalatia 3:16, na msome jambo hili, na tuone sasa hiyo ahadi ni nini, na tuone vipi kama-kama sisi ni ahadi Yake ama sivyo, 3:16. Sikilizeni hapa. Vema. Nitasoma kifungu cha 15, pia.

*Ndugu zangu, nanena kwa jinsi ya kibinadamu.  
Lijapokuwa ni agano la mwanadamu, hata hivyo  
likiisha kuthbitika, hakuna mtu alibatilishaye, wala  
kuliongeza neno.*

*Basi ahadi zilinenwa kwa Ibrahimu na kwa mzao  
wake, mzao (m, z, a, o), ahadi ilifanywa kwa mzao wake.*

“Kwa Ibrahimu na Mzao wake.” Sasa angalia.

*Hasemi, Kwa wazao, (wingi), kana kwamba ni wengi,  
bali kana kwamba ni . . . mmoja, kwa mzao wako, yaani,  
Kristo.*

<sup>417</sup> Basi, Kristo alikuwa Ndiye ule Mzao wa Ibrahimu. “Nasi tukiwa wafu katika Kristo, na kubatizwa katika Mwili Wake, tu Mzao wa Ibrahimu, na ni warithi wa ile ahadi.” Basi imekuwaje, utaangukaje, kama Mungu alikupa ahadi? Utarudi

nyuma vipi, na uondoke na ikulazimu kwenda jehanamu kwa ajili ya jambo hilo?

<sup>418</sup> Sasa, mnasema, “Vema, je! hatuwezi kurudi nyuma?” Kabisa. Na wakati unaporudi nyuma, utajuta, usiwe na wasiwasi. Ibrahimu alijuta, na hao wengine walijuta, na wewe utajuta. Usifikiri inakupa ruksa ya kutenda dhambi. Haikupi. Utalipia kila kitu unachofanya. Utavuna unachopanda. Unafanya dhambi moja ndogo nawe utavuna pipa zima lililoja. Hiyo ni kweli. Lakini, ndugu, hiyo si kusema kwamba umepotea. Hiyo ni kweli kabisa. Ibrahimu alivuna yale hasa aliyopanda. Hiyo ni kweli. Lakini angali alikuwa ameokoka.

<sup>419</sup> Lile agano ambalo Mungu alifanya na Israeli: walipoteza urithi wao, waliipoteza nchi ya ahadi na wakashuka kwenda Misri, bali hawakuwa wamepoteza agano lao. Mungu alisema, “Ninakumbuka ahadi Yangu kwa Ibrahimu. Ninakumbuka, nami nimeshuka kuja kuwakomboa watu Wangu. Shuka uende kule, Musa, na umwambie Farao, nilisema, ‘Achilia watu Wangu waondoke.’ Ninakumbuka nilifanya ahadi kwa Ibrahimu na kwa mzao wake.”

<sup>420</sup> Hivyo ndivyo ilivyo na kwetu sisi. Kwa hiyo kama wewe umekufa, na uhai wako umefichwa katika Mungu, kwa njia ya Kristo, hakuna kitu ulimwenguni kinachoweza kukugusa. Sasa, huenda ukaenda na kufanya makosa, bali kama wewe hakika, kweli, ni mwana wa Mungu, nawe unaona umefanya kosa, utaamka na kujaribu tena. Hiyo ni kweli, wala hutabaki pale.

<sup>421</sup> Lakini kama wewe ni mwoga, kama wewe ni kwekwe, kama hakuna “kuamka” kwako, utasema, “Aa, vema, hakukuwa na lolote kwenye jambo Hilo, hata hivyo.”

<sup>422</sup> Ufalme wa Mungu ni kama mtu aliyechukua jarife na akaenda baharini, akaitumbukiza ndani. Alipolivuta, alipata kasa, vyura, nyoka, mijusi, buibui, na samaki. Hiyo ndiyo Injili wakati inapohubiriwa.

<sup>423</sup> Kama vile Bwana tuseme atakavyomwambia mhudumu, kama Ndugu Graham, “Panda uende mahali *hapa*.” “Nenda *hapa* pemberi ukavue kidogo, Ndugu Graham.” Vema, anachukua jarife lake na anapanda anaenda kule na kuanza kuvua samaki.

“Unaenda wapi, Ndugu Bill?”

“Ninatoka kwenda mahali fulani pengine, na kutupa upande *huu*.”

<sup>424</sup> Ninavuta. “Hao hapo, Bwana. Wewe unajua hao ni nini.” Ninavuta jarife tena, “Vema, hawa hapa, Bwana.”

<sup>425</sup> Sasa, huyo kasa alikuwa ni kasa, kwanza. Ulishikwa tu katika jarife. Hiyo ni kweli. Na hivyo ndivyo watu wanavyoshikwa katika mhemuko, “Loo Haleluya! Haleluya!

Bwana asifiwe. Utukufu kwa Mungu. Haleluya!” Walishikwa tu katika jarife, ni hivyo tu.

<sup>426</sup> Kama ile roho ya kale ya Kasa imo ndani yao, haitachukua muda mrefu wao kusema, “Vema, ninakwambia . . .” Huyu hapa anaenda, anatambaa akirudi alikotoka.

<sup>427</sup> Naye maskini bibi Kamba wa maji baridi atasema, “Lakini mimi siwezi kuelewa na Hilo kabisa.” Unaona?

<sup>428</sup> Bibi Buibui ataketi pale kidogo, anaenda “plop, plop, plop,” anarudi moja kwa moja alikotoka, “Vema, hilo halikuwa na kitu chochote, hata hivyo.”

<sup>429</sup> Bibi Nyoka atasema, “Loo, hao ni kundi la watakatifu wanaojifingirisha. Hivyo ndivyo hasa jambo Hilo liliyio. Nitashuka niende kule kwa watu walio na akili timamu kuliko hiyo.” Mbona, kwanza, wewe ni nyoka. Jarife la Injili likushika tu, hakuna cha zaidi.

<sup>430</sup> Bali samaki anapelekwa mezani kwa Bwana. Yeye alikuwa ni samaki, kwanza. Mbegu yake ilikuwa ni samaki. Alianza, akiwa ni samaki, na Mungu alimjua samaki Wake tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Haleluya!

<sup>431</sup> Kumbuka, wote wanapumua maji yale yale kule yenye matope. Wote wanapumua kwenye kijito kile kile. Hiyo ni kweli. “Wote tulifanikiwa . . . kuunywea Mwamba ule ule wa kiroho. Wote walikula mana jangwani.” Kalebu na Yoshua walikula mana ile ile ambayo—ambayo wengine wao walikula. Na hao wote walianguka nyikani. Bali kulikuwako na wawili walioteuliwa kuingia, nao waliingia. Hiyo ni kweli.

<sup>432</sup> “Sote tumenyweshwa kutoka kwenye Chemchemi ile ile.” Bali si wote wanaokunywa wameokolewa. Sote tulifanywa kupaza sauti pamoja. Sote tumefanywa kushangilia pamoja. Lakini Wateule wameokolewa. Uliwahi kuona? Lilisema, “Hizo roho mbili, katika siku za mwisho, zingefanana sana hata zingewapoteza walio Wateule *kama* *yamkini*,” *kama* *yamkini*. Unaona? Hiyo ni Roho halisi ya Mungu, iliyoteuliwa kwa ajili ya Uzima wa Milele.

<sup>433</sup> Sasa tunafunga. Baadaye Ndugu Neville ataanzia mahali hapa nilipoachia. Vema.

*Nisemalo ni hili; agano liliothibitishwa kwanza na Mungu katika Kristo, torati iliyotokea miaka mia nne, miaka mia nne na thelathini baadaye, hailitangui, hata kuibatilisha ile ahadi.*

Hiyo ndiyo ahadi Mungu aliyompa Ibrahimu, kabla hata torati hajapata kuwako.

*Kwa maana . . . kwa kuwa urithi ukiwa kwa sheria, hauwi tena kwa ahadi; lakini Mungu alimkirimia Ibrahimu kwa njia ya ahadi.*

Si kwa kitu chochote ufanyacho, si kwa sheria zozote, sheria zozote za kanisa lako, kwa kijiungu na kanisa, wala kwa sheria nyingine yoyote. Ni tendo la neema ya Mungu kabisa, kwako. Haya basi.

<sup>434</sup> Angalia.

*Torati ni nini basi? Iliingizwa kwa sababu ya makosa,  
hata aje huyo mzao aliyepewa ile ahadi; . . .*

Hilo si ni dhahiri tu kama pua iliyoko usoni mwangu? “Iliingizwa, ipate kutumika hata aje yule Mzao, ambaye alikuwa ni Kristo, aliyepewa ile ahadi.”

*. . . iliamriwa kwa utumishi wa malaika kwa mikono  
ya mjumbe.*

*Basi aliye mjumbe si mjumbe wa mmoja; bali Mungu  
ni mmoja.*

<sup>435</sup> Sasa, ninaachia kuanzia papa hapa, kusudi Ndugu Neville aanzie papo hapo, kwa Jumatano hii ijayo.

<sup>436</sup> Sasa je! Mnaelewa na yale tuliyosema? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ya kwamba haiwezekani kabisa kwa Mkristo aliyezaliwa mara ya pili ambaye. . . Simaanishi, sasa, *anayeqiita* mwenyewe, “amezaliwa mara ya pili.” Ninamaanisha, Mkristo halisi, aliyezaliwa mara ya pili, kuanguka kamwe kutoka katika neema, hawezi kufanya hivyo. Anaweza kuanguka, hiyo ni kweli, bali hawezি, kamwe, kutoka kwenye neema hiyo.

Ibrahimu alianguka kutoka kwenye neema. Hakika, alianguka. Mungu alimwambia “kaa hapo.” Alitoka pale, bali kamwe hakupoteza agano lake. Alikuwa angali ni mteule wa Mungu. Alikuwa ni nabii akiwa ameketi pale. Sikuzote alikuwa ni nabii. Atakuwa ni wa Mungu daima.

<sup>437</sup> Sasa angalieni. Biblia ilisema, ya kwamba, “Israeli wote wataokolewa.” Ni wangapi wanaojua jambo hilo? Biblia ilisema, “Israeli wote wataokolewa.” Sasa, “Israeli si Israeli ambayo ni ya kimwili, bali ni Israeli ya Roho, kwa kuwa karama na miito havina majuto.” Je! hivyo ndivyo Biblia ilivyosema, kifungu kinachofuata hasa? Wagalatia. Vema. “Israeli wote wataokolewa. Kila mmoja wao ameokolewa.” Tunakuwaje Israeli? “Tukiwa wafu katika Kristo, tunakuwa Uzao wa Ibrahimu, nasi ni warithi kulingana na ahadi.”

<sup>438</sup> Paulo alisema, “Kile kilicho kwa nje si Myahudi, bali ni kile kilicho moyoni, ndicho kilicho Myahudi, Wale walioahidiwa.” Nasi ni Mzao wa Ibrahimu, kwa ile ahadi, kwa njia ya Kristo, tulimkubali Yeye kama Mwokozi wetu binafsi.

<sup>439</sup> Loo, ninatumaini mnalionia. Ninatumaini mnalipata, kama mnaweza kulishikilia kwa muda kidogo. Sasa hapa tunamalizia hili, ndipo tuanze na Melkizedeki, ambalo linarejea moja kwa moja kulileta hili tena. Tunaanza moja kwa moja kwenye. . . Loo,

ni ninii tu, jambo hilo lote ni zuri sana. Lakini tunaendelea tu kuingia katika mambo hayo matamu sana.

<sup>440</sup> Sasa, angalia, kama ungalichukua Hili hapa, linaonekana kama, kama ungalilisoma kutokana na kulitazama tu... Kama vile mtu mgumu kabisa wa utatu, ambaye anaamini ya kwamba kuna Miungu watatu, alivyoniambia wakati mmoja, ya kwamba, "Mathayo 3 ilisema kwa uhakika kabisa ya kwamba kulikuwako na watatu, Watu watatu mbalimbali katika Uungu."

<sup>441</sup> Nikasema, "Sina budi kuliona."

<sup>442</sup> Akasema, "Angalia." Akisimama papa hapa kwenye mimbara hii, alisema, "Angalia hapa, Mathayo 3." Kasema, "Wakati Yesu alipotoka moja kwa moja majini, tazama, mbingu zilimfungukia. Naye akamwona Roho wa Mungu kama hua. Ndipo ile Sauti kutoka Mbinguni ilikuwa ikisema, 'Huyu ni Mwanangu, mpPENDWA Wangu, ninayependezwa sana Naye.' Na kulikuwako na watatu: Mwana akiwa ukingoni; Roho Mtakatifu katikati; na Baba huko juu."

Nikasema, "Ndugu, Maandiko hayasomeki *hivyo*."

"Loo, ndio, yanasonicka *hivyo*."

Nikasema, "Sasa yasome tena, uone kama yanasonicka *hivyo*."

<sup>443</sup> Sasa, haya hapa maelezo ya huyo mtu. *Huyu* hapa Mungu, Mwana; *yule* pale Mungu, Baba; *huyu hapa* Mungu, Roho Mtakatifu, kama hua. Sasa, angalia. Biblia ilisema, wakati Yesu alipobatizwa. "Mwana alitoka moja kwa moja kutoka majini, tazama, mbingu juu Yake zilifunguka. Na Sauti ikisema kuhusu... Yeye alimwona Roho wa Mungu, Roho wa Mungu, kama hua." Si Mtu mwininge *huko* juu, bali Roho *huyu* wa Mungu alikuwa ndiye Huwa aliye kuwa juu Yake. Na Sauti ikija, ikisema, "Huyu ni Mwanangu, mpPENDWA Wangu, ambaye ninapendezwa kukaa ndani Yake." Sasa soma Mathayo 3 uone kama haisemi *hivyo*. Unaona? Si watu watatu, hata kidogo.

<sup>444</sup> Na hiyo ndiyo sababu. Hili halisemi haiwezekani kwa mtu kurudi, wakati akirudi nyuma. Halisemi *hivyo*. Halisemi *hivyo*. Linasema, "Haiwezekani kwa mtu kurudi kujifanya upya, baada ya yeye kuwa kule." Hawezi kufanya *hivyo*.

<sup>445</sup> Biblia ilisema, "Yeye aliyezaliwa na Mungu, hatendi dhambi, kwa kuwa hawezi kutenda dhambi. Kwa kuwa uzao wa Mungu unakaa ndani yake, wala hawezi kutenda dhambi." Ninaweza je kuitwa mwenye dhambi, wakati kuna dhabihu iliyoko pale kupachukua mahali pang? Ninaweza je kufa, wakati kifo kimelipwa kwa ajili yang? Ninaweza je kufa, wakati nina Uzima wa Milele? Ninaweza je kufanya jambo hilo? Huwezi kufa.

<sup>446</sup> Ningeweza je kupewa ruhusa iliyoandikwa kutoka kwa meya wa jiji hili, niendeshe gari mwendo wa maili sitini kwa saa humu jijini, na afisa ye yeyote anishike kwa kuendesha maili sitini

kwa saa? Unawezaje kufanya jambo hilo? Nina ruhusa kutoka kwa meya inayosema kwamba ninaweza kufanya hivyo. Hawezi kunitia mbaroni. Ninii—kukamata kwake... Angeweza kupiga filimbi na kila kitu, nami ningepuuzia tu jambo hilo. Haina maana yoyote; nina ruhusa.

<sup>447</sup> Nami ninawezaje, basi, kama Kristo akiisha kunifia nami nimekuwa haki Yake kwa sababu ya neema Yake na upendo Wake kwangu? Ninawezaje kutenda dhambi, wakati kuna kitu fulani kilichoko kati yangu na Mungu, dhabihu? Siwezi kutenda dhambi. Siwezi kufanya hivyo. Mungu kamwe hanioni; Yeye anamwona Kristo. Yeye anasimama mahali pangu. Na ninapofanya kosa lolote, Kristo hupachukua mahali pangu. Nilitubu, “Nimekosa. Yeye ni mwenye haki. Bwana, unajua moyo wangu. Unajua kama ninamaanisha jambo hilo ama silimaanishi. Nami nimekosa. Nisamehe.” Mungu halioni kamwe. Damu ya Yesu imenifunika, wakati wote. Basi Mungu anawezaje wakati wowote kuniona? Dhambi inawezaje ku—kuhesabiwa kwangu, wakati Mungu hawezি kufanya jambo hilo? Mara tu ninapofanya jambo hilo, limesamehewa. [Ndugu Branham anadata kidole chake—Mh.] Hiyo ni kweli.

<sup>448</sup> Ni kama tu kuchukua kitonesha kimoja ki—kidogo namna *hii*, kitonesha kidogo cha jicho, na kukichukua kimejaa wino mweusi na kukishikilia juu ya pipa la dawa ya kutakatisha, na kukitonesha tu mle ndani, na kisha kujaribu tu kukipata tena. Kinageuka tu kuwa dawa ya kuondoa madoa. Huo wino unabadiлиka unakuwa hiyo dawa. Na hivyo ndivyo, dhambi zako zilizotubiwa, kama uko ndani ya Kristo. Kati yako na Mungu kuna pipa zima la dawa ya madoa, na dhambi yako inakuwa haki kwa sababu Dhabihu isiyo na hatia inakungojea pale.

Nitakapofika mtoni mwisho wa siku,  
Na pepo za mwisho za huzuni zimevuma;  
Kuna wazo moja linalonichangamsha na  
kuufurahisha moyo wangu,  
Haitanilazimu kuvuka Yordani peke yangu.

<sup>449</sup> Hilo ndilo jambo moja zuri. Hilo ndilo jambo moja zuri. Haitanilazimu kuuvuka. Moja ya siku hizi, tutafikia mwisho wa safari yetu. Jua litakataa kutoa nuru yake, ndipo Mungu ataita.

<sup>450</sup> Adamu atanyosha mkono na kumtikisa Hawa, na kusema, “Mpenzi, hima. Wakati wa kuamka umefika.”

<sup>451</sup> Hawa atanyosha mkono amshike Habili, aseme, “Njoo huku, mpenzi. Wakati wa kuamka umefika.” Habili atamshika Sethi. Naye Sethi atamshika Nuhu. Nuhu atamshika... Loo, na kuendelea, moja kwa moja hata kwa Ibrahim, na kuendelea mbele wakiwa wanakuja. Kutakuwa na tetemeko kubwa na kuzinduka wakati Mwana wa Mungu atakapokuja. Tutasimama katika sura Yake siku hiyo.

<sup>452</sup> Sasa, kama ukitenda dhambi hapa, utailipia. Nime-...

<sup>453</sup> Linaendelea kuja niani mwangu, sina budi kulisimulia. Nimejaribu kulizima, mara nne ama tano. Sina budi kulisema. Ni wangapi wanaomkumbuka ndugu huyu, mchungaji, aliyeokuwa yuko hapa kwenye kanisa la Mungu? Ndugu, papa hapa, jina lake lilikuwa ni nani? Alifanya kazi kwa Vorgang kule chini. Loo, ninyi nyote... Kanisa la Kwanza la Mungu, papa hapa pembeni. Au, alikuwa akiuza za Rawleigh katika wakati wa—wa kuzorota kwa uchumi. Mtu mcha Mungu sana na mtakatifu. Ndugu Smith alipachukua mahali pake pale. Nitakumbuka jina lake mnamo dakika chache. Alikuwa ni mtu aliyeokolewa na Mungu.

<sup>454</sup> Kumbukeni, kama hutaki kurudiwa, na unafanya jambo bayo kama Mkristo, Mungu atakuonya. Na basi kama hutasi kia hilo onyo, Yeye atakuchukua tu akuondoe duniani. Hivyo ndivyo alivyofanya.

<sup>455</sup> Mnakumbuka, katika Biblia? Angalieni lile kanisa la Wakorintho. Aliwaambia kile walichokuwa, nafasi yao, katika Kristo. Lakini aliwaonya juu ya yale yatakayotukia. Nao wakajisahihisha, wakaweka mambo sawa, na Mungu.

<sup>456</sup> Basi maskini ndugu huyu, alikuwa maskini ni ndugu mzuri sana, ninaamini, Mtu aliyeokolewa na Mungu. Naye alijipatia kazi hapa kwenye ninii... ya Vorgang. Kama baadhi ya familia yake wameketi hapa, natumaini hamfikiri ya kwamba mimi... Siwajui ninyi kama mmeketi hapa. Lakini, Ramsey, Ndugu Ramsey, ni wangapi wanaomkumbuka Ndugu Ramsey juu hapa kwenye kanisa la Mungu? Hakika, mnakumbuka, maskini mtu mzuri sana. Naye alikuwa na mazoea ya kuja nyumbani kwangu nasi tungezungumza pamoja, nasi tungeketi pale na kulia na kushikana mikono; Mkristo halisi.

<sup>457</sup> Siku moja nilishuka nikaenda kule, ndio kwanza nitoke kwenye mkutano wa nchi za ng'ambo, niliweka gari langu lichekiwe, Ndugu Ramsey akasema, "Nikusaidie nini, Billy?"

<sup>458</sup> Nikasema, "Licheki, Ndugu Ramsey. Badilisha oily."

<sup>459</sup> "Sawa," akasema, "sawa, safi sana." Kasema, "Je! ulikuwa na mkutano mzuri?"

<sup>460</sup> Nikasema, "Loo, Ndugu Ramsey, ulikuwa ni mzuri sana." Nikasema, "Laiti ungeweza kwenda pamoja nami siku moja. Mbona usiende pamoja nami?"

Akasema, "Simtumikii Bwana tena, Billy."

Nikaangalia huku na huko, nikasema, "Ati umesema nini"

<sup>461</sup> Kwa namna fulani akasema tu, "Simtumikii Yeye tena," akaondoka akaenda zake.

<sup>462</sup> Nikawazia, "Loo, yeye ananitania tu." Nikaendelea, nikaenda mahali fulani.

<sup>463</sup> Nikarudi na nikaingia kwenye gari langu. Nikaja nyumbani. Nikaanza kuwazia juu ya jambo hilo, "Simtumikii Bwana tena."

<sup>464</sup> Bwana akaliweka moyoni mwangu kurudi nikamwulize tena. Kwa hiyo. Nikasema, "Meda, hebu angalia nyumba."

<sup>465</sup> Ndipo nikaingia, na nikaingia kwenye gari langu na kushuka kurudi kule tena, nikasimama tena, nikaingia kwa Vorgang. Nikasema, "Ndugu Ramsey, ninataka kukuuliza swalii."

Akasema, "Vema, Billy, ni swalii gani?"

Nikasema, "Ulisema, muda mfupi uliopita, humtumikii Bwana tena. Ulikuwa ukinitania tu, sivyo?"

Akasema, "La."

Nikasema, "Ndugu Ramsey, hu—humaanishi jambo hilo."

Akasema, "Ninamaanisha."

Nikasema, "Hivi humpendi?"

Akasema, "Kama ningalimpenda, ningemtumikia. Sivyo, Billy?" akaondoka akaenda zake.

Nikawazia. "Jamani, Ndugu Ramsey!"

Kasema, "Sitaki kuzungumza tena juu ya hayo."

<sup>466</sup> Nikaenda nyumbani, nikaingia chumbani, nikafunga mlango. Na, loo, unajua jinsi unavyoingiwa na huzuni kuu, kama kwamba ulikuwa umemnyang'anya mtoto mdogo biskuti ama chochote kile, unajua. Ni—nikawazia, "Kweli? Haiwezekani. Kweli jambo fulani limempata Ndugu Ramsey."

<sup>467</sup> Na kuna maskini mvulana mdogo mweusi, anayeitwa Jimmy, ye ye anahudhuria hapa kanisani. Ana mguu mmoja, mnajua; anachechemea, kidogo. Ninasa hau jina lake, anafanya kazi kule chini kwa Vorgang, anaendesha gari la kukokota magari yaliyoharibika. Alikutana nami, na akasema, "Unajua, Kasisi Branham," akasema, "Mimi simwelewi huyu Dkt. Ramsey wa hapa jirani." Akasema, "Nilimwambia, hivi majuzi, nikasema, 'Sote tulio gopa hata kusema neno lolote mahali hapa.' Nilimwambia, 'Wewe ulikuwa ni mtu anayemcha Mungu.' Lakini," kasema, "Alichukua cheti chake cha mhubiri na akaenda kwenye kikapu na kukichanachana, na kutupa vipande vyake kwenye kikapu, akasema, 'Sitaki kuwa na uhusiano wowote na jambo hilo tena.'"

Akasema, "aisee, bwana!" Nikasema. "Haikupasi kufanya hivyo."

Akasema, "Loo, Jim, nimeachana na kumtumikia Bwana."

Kwa hiyo akaendelea, nikasema, "Humaanishi hivyo."

<sup>468</sup> Naye akasema, "Basi akaniambia, kasema akawa anashuka aje kusaga vali zake, kwenye Siku ya Wafanya Kazi," nafikiri ndivyo ilivyokuwa. "Naye akasema, 'Sasa, nataka uje unisaidie, Jim.'"

<sup>469</sup> Akasema, “Nitakusaidia nikishatoka kanisani, lakini kwanza ninaenda kanisani.”

<sup>470</sup> Akasema alirudi kule chini, “Na Bw. Ramsey alikuwa akisaga vali za gari lake. Akasema, ‘Jimmy, chopoka uvuke mto. Hapa baa zimefungwa. Chopoka uvuke mto ukaniletee sanduku la bia.’”

<sup>471</sup> Akasema, “Bw. Ramsey, nimekuwa na hatia ya mambo mengi, bali kamwe sitakuwa na hatia ya kumpletea mtumishi wa Bwana sanduku la bia.” Akasema, “La, bwana. Kamwe sitafanya hivyo.”

<sup>472</sup> Naye akasema, “Vema, nenda tu. Kalileté, Jim.”

<sup>473</sup> Akasema, “Bw. Ramsey, ninasaga vali zako, lakini kama unataka kuleta bia yoyote, utaenda ukajiletee mwényewe.” Akasema, “Kamwe sitampletea mtumishi wa Bwana kitu kama hicho.”

<sup>474</sup> Kwa hiyo Ramsey akaruka na kuingia kwenye gari la Jimmy, akavuka mto, akarudi, nusu mlevi, akiwa na sanduku la bia, akiinywa.

<sup>475</sup> Akaanza kudhoofika, kisha akashikwa na ugonjwa. Unaona? Mungu asingeweza kusema naye. Mimi nilimwonya, nilifanya kila kitu nilichoweza. Ndugu Smith alimwendea akamwonya. Kila mtu alijaribu kufanya kila walichoweza kwa ajili yake. Hata hivyo, alitikisa tu kichwa chake. Nini kilitukia? Alishikwa na ugonjwa akafa. Hiyo ilionyesha ya kwamba alikuwa ni mtu aliyeokoka. Kama Mungu asingeweza kumfanya...kumihiisa, itambidi Yeye kumtoa duniani na kumpeleka Nyumbani. Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema hasa. Hivyo ndivyo Biblia inavyoahidi. Usipotaka kusahihishwa, itakubidi kuja Nyumbani.

<sup>476</sup> Kwa hiyo Mungu hawezi kukupoteza baada ya Yeye kukuokoa, bali anaweza kufupisha siku zako hapa, na kukufanya ujutie kila dhambi uliyotenda. Kwa hiyo, kama ukitenda dhambi, utayajutia yale uliyofanya. Kumbuka hilo tu.

<sup>477</sup> Sasa, sasa Bwana awe pamoja nanyi. Ninaamini, usiku wa leo, ya kwamba Ndugu Ramsey alikuwa ameokoka. Kweli kabisa, ninaamini jambo hilo. Lakini asingemtii Mungu kamwe, na wakati asingemtii Mungu, ilimbidi Mungu kumleta nyumbani. Hilo ndilo jambo pekee la kufanya, kwa sababu, ilikuwa ni nini? “Angeleta fedheha na aibu kwa Damu iliyomtakasa.” Hiyo ni kweli? “Na kulihesabu lile agano kuwa ni kitu kisicho kitakatifu,” kama hivyo sivyo hasa waraka huu wa Waebrania ulivyosema, Unaona? Isingewezekana kwake kupotea, bali angeleta fedheha na aibu, kwa hiyo itamlazimu Mungu kumwondoa duniani na kumleta Nyumbani. Hilo ndilo hasa lilitotukia.

Sasa Bwana na awabariki, tunapoinamisha vichwa vyetu kwa muda mfupi tu wa maombi.

<sup>478</sup> Sasa, Mungu aliye mtakatifu sana na Baba wa rehema, kwa kweli tunakushukuru kwa ajili ya ahadi tulio nayo, ya kwamba kamwe hutatuacha wala kututupa. Umeahidi utaambatana nasi kote maishani, na katika mauti utakuwa karibu nasi. Ulituahidi ya kwamba tulikuwa na Uzima wa Milele. Ulitupa sisi Huo bure. Hatuwezi kuupoteza kamwe. "Wote wajao Kwangu, wana Uzima wa Milele." Na kama ni Uzima wa Milele, hauna mwisho, Nawe uliahidi kutufufua katika siku ya mwisho. Tu wenye shukrani sana kwa ajili ya jambo hili. Tunashukuru kwamba Neno Lako linatufundisha jambo hili. Linatupa tumaini la hakika. Linatufanya tujue ya kwamba Baba yetu ni Upendo. Yeye anatupenda, Naye alituchagua. Ulisema, "Si ninyi mlionichagua Mimi, bali ni Mimi niliyewachagua na kuwaita." Nami ninakushukuru, Baba, ya kwamba umefanya hivyo. Na wengi wanaketi hapa, usiku wa leo, na ambaao wamekusudiwa Uzima wa Milele, na wamempokea Yesu Kristo kama Mwokozi wao binafsi. Na matunda ya Roho yanafuatana na maisha yao: wanana, wapole, wanyenyekemu, wenye upendo, furaha, amani, wavumilivu, wema. Tunashukuru kwa ajili ya hao.

<sup>479</sup> Nasi tunaomba, Baba, ya kwamba kama watakuwapo wengine hapa, usiku wa leo, ambaao hawana hayo matunda yakiambatana nao, bali wanategemea mazingaombwe fulani, kwa sababu walijichochea, siku moja, kwa maana walishikwa na mhemuko, waljisikia vizuri, huenda walipaaza sauti, huenda walifanya mambo mengi. Lakini, Baba, kama hawana tunda la Roho, linalowaweka kila siku katika upendo wa daima, wakiwasamehe adui zao, wakisahihisha makosa yao, na wakiishi wenye amani na wenye upendo, na wenye furaha na wakiwa wema wao kwa wao, na ni wenye bidii kwa ajili ya Kanisa, ni wenye upendo kwa Kristo na kwa watoto Wake, Ee Mungu wa Milele, wasamehe. Ingawa wanawenza kuwa ni wafuasi wa kanisa, washiriki wa mwili wa duniani, jalia waende sasa na kuwekeea kando kazi hizo za kimwili zisizo na uhai, na wakaze mwendo ili waufilikie utimilifu. Tujalie, Bwana. Jalia waje kwa Yeye aliye mkamilifu na wampokee kama upatanisho wao kwa ajili ya dhambi zao, ili Yeye apate kusimama akiwa dhabihu kamilifu kwa ajili ya mwanamume na mwanamke mwenye hatia. Pia awape neema Yake ya upendo na amani, hadi watakapoingia katika Uwepo wa Mungu wapate kuishi milele. Tujalie hayo, Baba.

Huku tumeinamisha vichwa vyetu:

<sup>480</sup> Kama kuna mtu kama huyo ambaye angetaka kubadilisha maisha yake ya sheria za jinsi ya kimwili, ya mabatizo, ya mihemuko, ya vitu vidogo vya kimwili kama hivyo, kwa moyo halisi uliojaa upendo halisi, ambapo—ambapo ungeweza kumwendea adui yako aliye mbaya sana, umkumbatie kwa mikono na kusema, "Ndugu, nitakuombea. Ninakupenda."

Kama ungetaka kubadilisha ujuzi huo wa mambo ya kimwili na ujuzi halisi wa upendo, je! ungeweza kumwinulia Mungu mkono wako? Na kusema, “Mungu, nichukue usiku wa leo, na unifanye kile ninachopaswa kuwa.” Nitakuombea, moja kwa moja kutoka hapa mimbarani. Je! ungetaka maombi? Inueni mikono yenu.

<sup>481</sup> Mungu akubariki huko nyuma, bwana. Mungu akubariki, ndugu. Mtu mwingine? Mungu akubariki, bwana. “Nimekuwa kanisani kwa miaka mingi.” Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki hapa, ndugu. Mungu akubariki wewe huko nyuma, bibi mdogo. “Nitamwomba Mungu anipe amani.” Je! unaninii... Je! unaghadhabika sana? Wewe ni mgonjwa? Unatilia shaka? Una mvurugiko wa akili hapa na pale? Hivi unashangaa kama ni kweli ama si kweli? Unapomjia Kristo, je! unakuja kwa uhakika kabisa, moyo uliojaa upendo? Je! unamwendea bila woga wowote, ukisema, “Ninajua kwamba Yeye ni Baba yangu”?

<sup>482</sup> Wala hakuna hukumu, umepita kutoka mautini ukaingia Uzimani. Unajua jambo hilo. Na unayaona maisha yako: ni mwenye upendo, mwenye kusamehe, wewe una utu wema, una amani, ni mpole. Matunda yote haya ya Roho yanaambatana na maisha yako, kila siku. Na mara unapofanya jambo lolote baya, “Loo, jamani.” Mara tu linapokuja niani mwako, “umefanya jambo baya,” upesi unaliweka sawa, papo hapo. Usingojee dakika nyingine, nenda papo hapo na ukaliweke sawa. Usipoliweka sawa, vema, huna Roho wa Kristo. Huenda ukawa u mwanamke mzuri, huenda ukawa u mwanamume mzuri, huenda ukawa unaheshimika sana kanisani, huenda ukaheshimiwa sana na majirani, bali je! umeenda ukaufikia ule utimilifu, kufikia mahali pale ambapo unamtumainia Kristo kabisa? Na kwa jambo hili, anakupa muhuri. “Ibrahimu alimwamini Mungu, na ikahesabiwa kwake kuwa haki. Ndipo Mungu akampa muhuri wa tohara, kama thibitisho.”

<sup>483</sup> Sasa unasema, “Ninamwamini Mungu. Nilitubu.” Lakini je! Mungu alikupa muhuri wa Roho Mtakatifu, huko nyuma maishani mwako, wa upendo, furaha, matunda ya Roho, kuthibitisha ya kwamba umeokoka? Kama hajafanya jambo hilo, basi bado hajaitambua imani yako. Umefanya tu maungamo. Yeye hajaikubali, kuna kasoro fulani. Je! ungetaka kumpokea Yeye, basi? Inua mkono wako, kama kuna mtu mwingine, kabla hatujaomba.

<sup>484</sup> Mungu akubariki, bibi mdogo. Mungu akubariki wewe kule nyuma, pia. Mungu akubariki. Vema. Mtu mwingine, kabla tu hatujaomba? Vema. Mungu akubariki, kule nyuma, dada. Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki, ndugu yangu. Safi. Mikono kama kumi, kumi na tano imeinuliwa.

Sasa na tuombe.

<sup>485</sup> Bwana mtakatifu, wakiwa vitini mwao, wanasogea kwenye madhababu. Iko kwenye viti vyao, ambapo wameketi sasa, kwamba ulinena na mioyo yao, ya kwamba wao “wamekosa.” Ni hapo kwenye viti vyao ambapo Wewe umeweka shauku moyoni mwao, ya kwamba “wana shauku ya kufanana zaidi na Yesu.”

<sup>486</sup> Wanataka maisha yao yabadilishwe. Wanataka kuwa wapole na wanyenyekevu. Wanataka kuwa wanana waliojaa subira. Wanataka kuwa wavumilivu, wenye kuchukuliana. Wanataka kuwa sana kama Wakristo, wanafanana sana na Kristo, mpaka ulimwengu utasema, wanapotembea barabarani, “Yule mtu ni Mkristo kwelikweli. Mwanamke yule ni Mkristo kwelikweli. Loo, wao ni watu wanana sana, wapole sana, wacheshi sana!”

<sup>487</sup> Tujalie, Bwana, ya kwamba watapokea tukio hilo, usiku wa leo. Na jalia kamwe wasitumainie uwezo wa kanisa lao, uanachama wao na kanisa lolote, madhehebu yoyote; wala juu ya mihemuko yao, juu ya ono lolote, kama vile, jambo ambalo limetukia kwa kuhemukwa; labda walipaaza sauti, walinenza kwa lugha, ama kitu fulani kingine.

<sup>488</sup> Ee Mungu wa Milele, jalia wasijaribu kutumainia kufika Mbinguni juu ya mambo hayo, kwa maana tumeyaona hayo mara nyingi sana yakishindwa vibaya sana. Nawe ulisema yatashindwa, “Zikiwako lugha, zitakoma! Ukiwako unabii, utakoma. Yakiwako maarifa, yatakoma. Loo, vitu hivi vyote, ama hata karama, miujiza ya uponyaji, yote itabatilika. Ni huo upendo wa Kiungu tu ndio utakaodumu.”

<sup>489</sup> Mungu, umba huo moyoni mwao, na jalia wajue ya kwamba hiyo ndiyo ile Roho inayozaa hayo matunda. Fanya hivyo sasa hivi, Bwana, tunapokungojea Wewe, kwa maana tunayaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

<sup>490</sup> [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Mipira ya moto ikiruka, na kuona njiwa wakienda huku na huko jengoni, kumwona Kristo akiingia na miiba mikononi Mwake, na katika ninii Yake... Loo, ulijua ya kwamba hizo ni njama za mpinga-Kristo? Yeye alisema, “Mambo haya yatakapoanza kutimia, basi angalieni juu, ukombozi wenu unakaribia.” Basi hiyo ndiyo sababu ninapenda kuomba sana kila dakika niwezayo kwa kanisa, na kuwafanya imara. Ndugu Neville huenda asiwe nasi sikuzote. Ninamwamini Ndugu Neville kuwa ni mwalimu mzuri, na thabiti wa Injili. Hatujui ni kitu gani kitakachonyemelea kiingie kwenye mimbara hii, na, kitakapofika hapa, “Kondoo Wangu wanajua Sauti Yangu.” Dumuni na hilo Neno. Kamwe msiliache hilo Neno. Dumuni Nalo. Kaeni imara katika uhuru ambapo Kristo amewafanya huru. Msifungiwe nira hizo zote za utumwa na kadhalika. Simameni imara, na simameni mkiwa huru. Mungu atawabariki. Hatuna kitu ulimwenguni cha kuogopa.

<sup>491</sup> Daima mnashangaa. Ninaona watu wakija kuombewa, wataingia mstarini kwa wasiwasi. Wakati mwingine wanapoona kampeni ya uponyaji, wataingia kwenye mstari *huu*, wataenda kwenye mstari *huu*. Siwahukumu. Wanajaribu kupata faraja, bali wanaendea njia mbaya. Mnafanya kinyume chake, kile Mungu alichosema msifanye. Unaona? Unapokikaribia Kiti cha Enzi cha neema kwa ujasiri, na kuamini, ya kwamba, “Uliomba, utapata.” Kaa Nalo. Hivyo ndivyo inavyofanyika; si kutangatanga kutoka ufufuo mmoja kwenda katika mwingine, kutoka kanisa moja hadi lingine, kutoka kwenye mikutano moja hadi mwingine.

<sup>492</sup> Mbona, wameifanya hii mikutano ya uponyaji kama kundi la upuuzi. Bila shaka, wamefanya hivyo. Imefikia mahali ambapo watu wenyе akili, wanaangalia huku na wanashangaa hayo yote yana maana gani. Kitu kama hicho, Mungu hataki mambo hayo. Uponyaji si lazima uwe kwenye mikutano. Uponyaji unapaswa kuwa katika kila kanisa la mtaa fulani, karama hizi zote zikitenda kazi. Bali msije mkakwamia kwenye karama hiso. Msizijali kamwe hiso karama. Kama Mungu anataka kukutumia kwa jambo fulani, Yeye atafanya jambo hilo. Bali, mtafuteni Mpaji.

<sup>493</sup> Martin Luther, wakati mmoja baada ya kunena kwa lugha, aliulizwa kwa nini hakuhubiri hilo, akasema, “Kama ningehubiri hilo, watu wangu watakazana wapate hiyo karama badala ya Mpaji.” Hiyo ni kweli.

<sup>494</sup> Moody, wakati mmoja, akizungumza, na akaanza, wakati alipokuwa akihubiri sana chini ya upako, alinena kwa lugha. Akasema, “Mungu, nisamehe kwa kugugumiza maneno ya kipumbavu.” Kweli. Unaona? Nao walikuwa nayo mambo hayo. Tunaamini mambo hayo, bali yanapaswa kuwekwa mahali pao. Wala hayapaswi kuwekwa kama mathibitisho.

<sup>495</sup> Hakuna kitu hata kimoja kilichosalia katika Biblia, kama “thibitisho la Roho Mtakatifu,” ni matunda ya Roho tu. Tafuta mahali popote ambapo Yesu alisema hivyo. Naam, bwana. Thibitisho la Roho Mtakatifu ni tunda la Roho yako. Yesu alisema hivyo, “Kwa tunda lao mtawatambua.” “Na tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, wema, amani, utu wema, upole. Na tunda la adui ni uadui, chuki, kijicho, ugomvi, na kadhalika; hilo ndilo tunda la adui.” Kwa hiyo, unaweza kujua kwa namna unayoishi, mahali unaposimama na Mungu. Kama moyo wako wote unapendana Naye, nawe unampenda na ni mwanana, na unaishi Naye kila siku, unajua umepita kutoka mautini kuingia Uzimani. Kama sivyo, nawe uko vinginevyo, unamwiga tu Mkristo. Hiyo ni kweli. Ambapo, uigaji wote wa kimwili bila shaka utafichuliwa. Tunajua jambo hilo.

<sup>496</sup> Kwa hiyo, usiishi maisha ya aina hiyo, hailazimu kufanya hivyo. Kwa nini ukubali kibadala, wakati mbingu nzima huko

juu zimejaa mazuri na yaliyo halisi? Bila shaka. Hebu nimchukue Mungu, hilo ndilo ninalotaka. Amina.

<sup>497</sup> Sasa, kuna mtu yejote aliyejeku ili aombewe? Kama ulikuja uombewe, inua mkono wako. Tulikuwa na ibada ya uponyaji asubuhi ya leo. Ninawazia basi... Bibi huyu hapa? Vema, dada, unaweza basi kuja mbele? Na ndugu yetu, mzee, hapa, njoo sasa kwa ajili ya kupaka mafuta.

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

...niangazie;

Loo, niangazie, Bwana, niangazie,

Jalia Nuru kutoka nyumbataa iniangazie.

<sup>498</sup> Yeye si ni wa ajabu? Hebu na tuinamishe tu vichwa vyetu, komyakimya sana sasa. Na, *Niangazie*, tena. Haya, twendeni sasa, kila mtu, ambaye, “*Niangazie...*” Hebu mwabudu tu sasa nafsini mwako, unaona, mkiwa mmetulia. Ibada ya uponyaji inakuja. Ujumbe umekwisha. Na tuabudu.

Jalia Nuru kutoka nyumbataa iniangazie;

Loo, niangazie, Bwana, niangazie.

Jalia Nuru kutoka nyumbataa iniangazie.

Kuwa tu kama Yesu, kuwa kama Yesu,

Loo, duniani ninatamani kuwa kama Yeye;

Kote katika safari ya maisha toka duniani  
mpaka Utukufuni,

Ninaomba tu kuwa kama Yeye.

Tutatembea Nuruni, ni Nuru nzuri iliyoje,

Inakuja toka ambako matone ya umande wa  
rehema yanang’aa;

Tuangazie kote, usiku na mchana,

Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Enyi watakatifu wote wa Nuru tangazeni,

Yesu, Nuru ya ulimwengu,

Ndipo kengele za Mbinguni zitalia,

Yesu, Nuru ya...

Tupokee, Bwana, tunapokuabudu Wewe.

Tutatembea Nuruni, Nuru nzuri,

Inakuja toka ambako matone ya umande wa  
rehema yanang’aa;

Tuangazie kote, usiku na mchana,

Yesu, Nuru ya ulimwengu.

<sup>499</sup> Je! hampendi huko kusuguliwa sawasawa kabisa? Mnajisikia vizuri? Inua mkono wako, mwambie. Kuna kitu fulani kuhusu hizo nyimbo za mtindo wa kale, wimbo wa kale wa dini, afadhali niwe nazo kuliko hizi nyimbo mpya zote za kilimwengu zilizoingizwa, na ziko katika makanisa ya Kikristo. Ninaupenda ule wa kale, ninaupenda.

Yesu, unihifadhi, (Jamani!)  
 Hapa msalabani,  
 Wajiao Kalvari,  
 Waponywe Damuni

Msalaba, msalaba,  
 Loo, humu nina sifa  
 Hata nitapumzika  
 Mahali pa raha.

<sup>500</sup> Ningeweza kutoka kwenye mambo ya ulimwengu kwa urahisi sana wakati huo unapoimbwa. Nawe je! [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ni ajabu jinsi gani! Mambo yote yako sawasawa? Unajua, nina furaha tayari nimeyamaliza yote. Nawe je? [“Amina.”] Lile deni la kale lililipiwa, zamani sana. Nilimwambia, “Bwana, sitaki shida yoyote kule chini mtoni. Ni—nintaka kuwa na hakika sasa.” Ninataka kumjua Yeye. Ninataka kumjua Yeye.

<sup>501</sup> Kuna shimo kubwa lililowekwa, lenye giza mbele ya kila mmoja wetu. Tunaelekea huko. Kila wakati moyo wetu unapopiga, tunakaribia zaidi na zaidi. Lakini nitakapofika hapo, sitaki kufadhaika kama mwoga, nataka kujifunika kwa mavazi ya haki Yake, niingie humo, nikijua jambo hili, ya kwamba, “Ninamjua katika nguvu za kufufuka Kwake.” Kwamba, wakati Yeye atakapoita, nitatoka kutoka katika wafu. Jamani!

<sup>502</sup> *Yesu Kwa Imani*, na tuuimbe sasa.

Yesu kwa imani,  
 Nakutumaini,  
 Peke Yako.

Nisikie sasa,  
 Na kunitakasa,  
 Ni Wako kabisa,  
 Tangu leo.

<sup>503</sup> Sasa, Ewe Mwalimu mkuu, kama vile uliovyotufundisha katika Neno Lako la ajabu sana, miyo yetu inatetemeka tu, kwa neema ya kunyakuliwa, kujua ya kwamba tumepita kutoka mautini kuingia Uzimani. Yote ni kwa kupitia kwenye wema wa Bwana wetu Yesu, aliyetuuta, na ametuosha katika Damu Yake, na ametuweka mbele ya Kiti cha Enzi cha Mungu, bila hatia, bila lawama, kwa maana alizichukua dhambi zetu. Hatuna dhambi. “Mungu aliweka uovu wetu sote juu Yake, Naye alijeruhiwa kwa makosa yetu.” Loo, jinsi tunavyompenda, Mwana-Kondoo mkuu wa Mungu!

<sup>504</sup> Na tunaomba, Baba, ya kwamba Wewe utatupa sisi usemi, maneno, tupate kuwaambia wengine; wapate kumjua Yeye, pia, na kumpenda Yeye, kwa kuwa Yeye anawapenda. Tupe neema hii.

Pia asante, Baba, kwa ajili ya hao watoto wachanga waliozaliwa upya ambao ndio kwanza waingie katika ufalme wa Mungu. Jalia wapate kanisa zuri la nyumbani mahali fulani, na hapo wakutumikie mpaka kifo kitakapowaweka huru kutoka kwenye mwili huu wa kale wa maumivu makali na uchungu, na kanisa hilo liwakilishe mbele Zake, wasio na hatia, wasio na lawama, katika zama zijazo, wakiwa na Uzima wa Milele. Kwa maana tunaomba hayo katika Jina Lake. Amina.



## *KITABU CHA WAEBRANIA*

Jumbe hizi kumi na moja za Ndugu William Marrion Branham zilizohubiriwa hapo awali katika Kiingereza kutoka tarehe 21 Agosti mpaka tarehe 22 Septemba, 1957, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, U.S.A., zimetolewa kwenye kanda za sumaku zilizorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings. Ilachapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2009 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

[www.branham.org](http://www.branham.org)

## **Ilani ya haki ya kunakili**

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

**VOICE OF GOD RECORDINGS**  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)